*Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Tano - Tarehe 21 Machi, 2015**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu!

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

***Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi Ghalani wa Mwaka 2014 (The Warehouse ReceiptS( Amendment) Bill, 2014)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghalani wa Mwaka 2014 *(The Warehouse Receipts (Amendment) Bill, 2014)* sasa usomwe mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana wewe binafsi, Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara na Mwenyekiti mwenza na Wajumbe wa Kamati ya Kilimo Mifugo na Maji, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wadau wa mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa mapendezo na maoni yao ya kurekebisha sheria hii kwa lengo la kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa Stakabadhi za Ghala ni mfumo unaorasimisha matumizi ya bidhaa kwa kupata stakabadhi kwa ajili ya kuhifadhi, kufanya biashara na huduma za kifedha kama benki na kadhalika. Stakabadhi hiyo inaonesha umiliki, kiasi, ubora na thamani ya bidhaa husika. Mfumo huu ulipitishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 10 ya mwaka 2005 na kuanza kutumika rasmi mwaka 2007 baada ya Kanuni zake kupitishwa mwaka 2006. Hadi kufikia Desemba 2014, mfumo huu umetumika kwenye mazao ya korosho, kahawa, ufuta, alizeti, mahindi, mpunga na mbaazi na kuwezesha tani 950,000 za mazao kuuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria za Stakabadhi za Ghala yana lengo la kuboresha mfumo huu ili kuondoa upungufu uliojitokeza kwenye utekelezaji wa sheria ya mwaka 2005 ikiwa ni pamoja na kuweka masharti madhubuti zaidi ya takayowabana wadau watakaokiuka sheria hii na pia kuendana na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya kwa kiasi kikubwa yataondoa upungufu mwingi uliyojitokeza awali katika kutekeleza sheria hii muhimu yenye maslahi ya moja kwa moja

kwa wakulima. Marekebisho hayo pia yamezingatia hoja ya kwamba Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ni misingi katika kuanzisha *Commodity Exchange Program* ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili; Sehemu ya kwanza inaainisha masharti ya awali kama vile jina la sheria inayopendekezwa, na sehemu ya pili inaainisha marekebisho yanayopendekezwa kwenye vifungu mbalimbali vya Sheria ya Stakabadhi za Ghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho katika kifungu cha 2 yanalenga kupanua wigo wa sheria ili iweze kutumika pia kwa bidhaa zisizo za kilimo kama vile madini, gesi, mafuta na mazao ya misitu. Kwa sasa sheria inasimamia bidhaa za kilimo tu.

Kifungu cha 3 cha Muswada kinafanyiwa marekebisho ya tafsiri ya baadhi ya misamiati ili kuendana na marekebisho yanayopendekezwa kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4 cha Muswada kinafanyiwa marekebisho kwa lengo la kubadilisha jina la bodi kuwa Bodi ya Udhibiti wa Stakabadhi za Ghala ili iendane na majukumu mapana zaidi ya bodi hiyo kwa sasa.

Aidha, kuongeza masharti yanayomruhusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kati shauri lolote litakalofunguliwa dhidi ya Bodi ya Stakabadhi za Ghala kwa lengo la ama kuendesha shauri hilo au kutoa ushauri; hivyo kwa mujibu wa marekebisho yanayopendekezwa, bodi itakuwa na wajibu wa kumjulisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya shauri lolote litakalofunguliwa dhidi ya bodi.

Kwa mantiki hiyo Sheria ya Mwenendo wa Madai dhidi ya Serikali itatumika kwa kutoa taarifa ya nia ya kuanzisha madai dhidi ya Serikali. Taasisi nyingi za Serikali ikiwemo bodi hii kwa sasa hazina uwezo wa rasilimaliwatu na fedha kuendesha kesi zinazoweza kufunguliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5 cha sheria kinarekebishwa ili kuongeza majukumu ya Bodi ya Udhibiti wa Stakabadhi za Ghala kwa lengo la kuhakikisha kuwa bodi inakuwa na wajibu wa kujenga mahusiano baina yake na taasisi nyingine za kitaifa na kimataifa, na pia kuiwakilisha Serikali katika majadiliano yanayohusu stakabadhi za ghala ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6 cha Muswada kinarekebishwa ili kuipa bodi wajibu wa kupata ridhaa ya Waziri wa Fedha ili kuweza kukopa fedha kama taasisi nyingine za Serikali. Vile vile inapendekezwa kuanzisha kamati za kusimamia mfumo huu katika ngazi ya Mkoa na Wilaya au Miji chini ya Katibu Tawala wa Mkoa au Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya au Mji na zitatimiza wajibu wake kwa kuzingatia maelekezo ya bodi; utaratibu huo haumo kwenye sheria iliyopo sasa hivi.

Aidha Waziri mwenye dhamana atatayarisha kanuni kwa kumshirikisha Waziri mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) juu ya muundo wa kamati na kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 7 cha Muswada kinapendekeza kurekebisha kifungu cha 8 cha sheria iliyopo kwa lengo la kutoa kinga ya utendaji kazi wa bodi, jambo ambalo halikuwepo kwenye sheria ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 9 cha Muswada kinapendekeza kurekebisha kifungu cha 18 ili kuzuia mtu aliyepewa leseni ya kuendesha ghala chini ya mfumo huu kuitoa leseni yake kwa mtu mwingine bila kibali cha bodi. Lengo ni kuongeza udhibiti na matumizi sahihi ya leseni. Aidha Muswada unapendekeza adhabu ya faini isiyoungua milioni 20 au kifungo kisichopungua miezi 12 na sio zaidi ya miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 18 cha Muswada huu kinapendekeza kufanya marakebisho katika kifungu cha 36 cha sheria iliyopo kwa lengo la kubainisha mambo yanayoweza kusababisha stakabadhi za ghala kuwa batili. Mambo hayo ni pamoja na stakabadhi kutojazwa kwa ufasaha, kutosainiwa na kadhalika, lengo ni kuimarisha udhibiti wa mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 20 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 38 cha sheria iliyopo kwa kupunguza masharti yasiyo ya lazima na kuweka sharti la kutoa ripoti kwa bodi pale stakabadhi ya ghala inapopotea. Lengo ni kurahisisha zoezi la kutoa stakabadhi durufu *(duplicate)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada umependekeza kuwa na kifungu kipya cha 39(a) kinachowataka Mameneja Dhamana kuomba leseni kwa bodi. Lengo likiwa ni kuonesha kazi, haki na wajibu wao katika kutekeleza mfumo wa stakabadhi za ghala kama itakavyofafanuliwa katika kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 26 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 60 cha sheria kwa kuongeza kifungu kidogo cha pili kuiwezesha bodi kufanya tathmini ya mzigo na kuruhusu kiasi cha mzigo wenye thamani sawa na gharama za tozo *(lien)* anazodai mwendesha ghala kutoka kwa mweka mali aliyekataa au kushindwa kulipa tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu vya 29, 30 na 31 vya Muswada ni mapendekezo ya kurekebisha vifungu vya 71, 72 na 73 vya sheria ya sasa ili kuweka mfumo wa adhabu utakaoendana na wakati. Inapendekezwa faini iwe asilimia 50 ya thamani ya bidhaa zilizohusika katika kosa badala ya adhabu iliyopo ambayo imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 32 Muswada kinafanya matekebisho kwenye kifungu cha 75 kwa kuongeza kifungu cha (2) kuhusu sharti la mwendesha ghala kuwajibika kumfidia mteja wake pale itakapothibitika kuwa biadhaa zimetoka ghalani lakini hazijamfikia mteja. Fidia itakayotolewa itakuwa sawa na thamani zilizopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 33 cha Muswada kinafanya marekebisho kwenye kifungu cha 78 ili faini kwa mtu yeyote aliyefanya kosa kulipa faini isiyo chini ya shilingi milioni 5 na isiyozidi milioni 10 au kifungo kisichopungua miezi 12 na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja katika kosa husika. Lengo ni kupunguza makosa chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya sheria hii inaweka kifungu kipya cha 70(a) ili kuanzisha Jukwaa Rasmi la Mauzo na kutaka mazao yote katika mfumo wa stakabadhi ya ghala yauzwe kupitia jukwaa hilo. Lengo ikiwa ni kuweka miundombinu ya kuuza bidhaa kwa ushindani na kuondoa udanganyifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 34 cha Muswada kinapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 78(a). Kifungu hiki kinaipa Bodi ya Stakabadhi za Ghala mamlaka ya kutoza faini kwa mtu anayetenda kosa chini ya sheria hii na kukiri kosa na kuwa tayari kulipa faini husika

papo kwa papo. Lengo ni kuongeza kasi ya utatuzi wa migogoro badala ya mfumo wa Mahakama za kawaida zinazochukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 36 cha Muswada kinapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 80, 81 na 82. Vifungu vya 80 na 81 vinatambua mamlaka ya taasisi zinazohusika na viwango na mizani kuwa viwango hivyo vitatumika katika mfumo wa stakabadhi za ghala.

Kwa upande mwingine kifungu kipya cha 82 kinaweka masharti yanayotambua leseni na stakabadhi za ghala zitakazotolewa kwa njia ya kielektroniki. Lengo ni kuhakikisha kuwa mfumo unaenda na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Bunge lako Tukufu litapitisha Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Mheshimiwa Rais akaridhia, changamoto zilizokuwa zinaukumba mfumo huu zitaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Hoja imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kitandula!

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Aprili 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumi ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi za *Ghala (The Warehouse Receipt Amendment)* ya mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 14 Januari, 2015, Waziri wa Viwanda na Biashara aliwasilisha mbele ya Kamati Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala *(The Warehouse Receipt Amendment*) ya mwaka 2014. Katika kikao hicho Kamati ilijulishwa kwamba sheria hii ina mabadiliko makuu manne ambayo ni wajibu wa bodi, utaratibu wa kuuza mazao, viwango vya adhabu na matumizi ya viwango mbalimbali katika mfumo.

Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi za Ghala yana lengo la kuboresha mfumo uliopo ili kuondoa upungufu uliojitokeza kwenye utekelezaji wa sheria inayorekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84 na Kanuni ya 117 ya Kanuni za Bunge toleo la Aprili 2013, tarehe 15 Januari, Kamati ilipata fursa ya kuwasikiliza wadau mbalimbali ili kutoa maoni yao. Michango ya wadau waliofika mbele ya Kamati imetoa mchango mkubwa katika utungaji wa sheria inayopendekezwa. Aidha kwa kuzingatia maudhui ya Muswada huu, Kamati yangu ilishirikiana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ili kupata maoni yake baada ya kupokea maoni ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau walioshiriki kutoa maoni yao ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maji, Bodi ya Korosho, Jukwaa la Wadau wa Sekta Binafsi, Chuo Kikuu cha *SUA* na *CBT*, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Kituo cha Sheria za Haki za Binaadamu, Bodi ya Pamba Tanzania, Baraza la Taifa la Kilimo na Bodi ya Nafaka Mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Muswada: Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ulianzishwa na Serikali kwa lengo la kupunguza kuyumba kwa bei ya mazao ya kilimo hapa nchini, changamoto ambayo imewasumbua wakulima kwa muda mrefu. Aidha, kutokana na kutotabirika kwa mwenendo wa soko na hivyo mazao kukosa bei ya uhakika, sekta ya kilimo kwa muda mrefu imejikuta ikikabiliwa na changamoto ya kutokopesheka. Benki za biashara zimekuwa zikikwepa kutoa mikopo kwa wakulima na hata pale mikopo hiyo ilipotolewa bado iliambatana na masharti magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuanzisha Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuwa mfumo huu umeongeza gharama kwa wakulima kupitia ulipaji wa tozo kwa kila kilo ya mazao inayonunuliwa na wakulima kulazimika kugharamia ulipaji wa mishahara kwa watunza maghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu pia umeonekana kuwa wa kinyonyaji hususan pale ambapo mazao ya mkulima yamekuwa yakikopwa na malipo kuchelewa kutolewa. Aidha mfumo huu pia unalalamikiwa kuwatenga wakulima wadogo kuwa na usimamizi mbovu na kukosekana kwa uadilifu miongoni mwa watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za Marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi za Ghala: Mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii yanalenga kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizobainika kwenye sheria inayofanyiwa marekebisho, hususan katika kumsaidia mkulima mdogo na wa kati kudhibiti upotevu na uharibifu wa kuhifadhi mazao kwenye maghala wakati wakisubiri yauzwe kwa bei nzuri. Sambamba na hilo, maboresho ya mfumo wa stakabadhi za ghala yatawezesha mkulima kutumia mazao yaliyopo ghalani kama dhamana ya kupata mikopo kutoka kwenye mabenki na taasisi nyingine za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine zinazotarajiwa kufuatia Marekebisho ya Sheria za Stakabadhi za Ghala namba 10 ya mwaka 2005 ni pamoja na kuwezesha Bodi ya Udhibiti wa Stakabadhi za Ghala kusimamia na kuratibu mfumo wa Stakabadhi za Ghala badala ya kutoa leseni pekee, kuweka mfumo wa kisheria wa kuuza mazao na bidhaa zilizohifadhiwa ghalani ikiwa ni pamoja na kuwezesha mfumo huu kutumika katika soko la mazao bidhaa *(commodity exchange)*, kuunganisha mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo na mfumo wa fedha ndani na nje ya nchi, kupanua wigo wa matumizi ya mifumo ya mazao ambayo sio ya kilimo, kurahisisha utatuzi wa migogoro inayotokana na matumizi ya stakabadhi za ghala, kupunguza masharti yasiyo ya lazima katika usimamizi wa mfumo, kuanzisha utaratibu mzuri wa utoaji wa adhabu zinazoendana na wakati na zinazotekelezeka na kuwezesha mfumo kuwa shirikishi katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada za Serikali zinazofanywa ili kuboresha Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Hata hivyo, Kamati inaamini kuwa ili Mfumo wa Stakabadhi za Ghala uweze kuleta mafanikio tarajiwa, lazima uboreshaji huu uende sambamba na kuwepo kwa jitihada za makusudi za kuanzisha viwanda kwa lengo la kuongeza thamani ya mazao hapa nchini. Ni kwa kufanya hivyo ndipo tutaweza kujihakikishia uwepo wa soko la uhakika na bei nzuri kwa mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati: Kifungu kipya cha 70(a) cha marekebisho ya sheria kinaipa mamlaka Bodi kuanzisha majukumu ya kuuzia mazao ya bidhaa chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Kamati inaona kuwa utaratibu huu sio sahihi na hivyo inapendekeza Mamlaka ya Mitaji ya Dhamana ndiyo ihusike katika kutoa idhini au leseni kwa majukwaa yote yatakayotumika kuuza mazao katika mfumo wa stakabadhi za ghala. Aidha Kamati inashauri kuwa Bodi kwa kushirikiana na Soko la Mitaji la Dhamana iweke utaratibu wa

kuunganisha mfumo wa stakabadhi za ghala na majukwaa ya kuuza mazao ya bidhaa yaliyopewa idhini au leseni na mamlaka hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza pia sheria iainishe muda mahsusi wa watu waliokuwa wakiendesha majukwaa ya kufanyia biashara kabla ya kuanza kutumika kwa sheria hii, kuomba leseni kwa Mamlaka ya Mitaji ya Dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukwepa uwezekano wa watu kufanya shughuli za stakabadhi kinyume na sheria na hivyo kuleta usumbufu kwa wananchi, Kamati inapendekeza sheria itamke wazi kuwa yeyote ambaye hatambuliki na sheria ya stakabadhi, haruhusiwi kutoa stakabadhi ya ghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kiongezwe kifungu kipya cha 39(a) ambacho kitamtambua Meneja wa Dhamana *(Collateral Manager)*. Kamati inaamini kutambulika kwa meneja wa dhamana kutaondoa uwezekano wa kutokea mchanganyiko wa kiutendaji kati ya mwendesha ghala na meneja dhamana. Aidha kifungu hiki kimpe Waziri mamlaka ya kutayarisha kanuni zitakazobainisha kazi, wajibu na haki za Meneja Dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6(c) "(a)" na "(b)" cha Muswada kinapendekeza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuongoza vikao vya Kamati ya Usimamizi wa Mfuko kwenye Mikoa na Wilaya; kirekebishwe kwa kuondoa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, badala yake Kamati inapendekeza nafasi hizo zichukuliwe na Katibu Tawala wa Mkoa na Mkurugenzi wa Halmashauri ambao ni watendaji wa Serikali. Kamati inaamini hatua hii itasaidia kutengenisha siasa na utendaji na hivyo kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 26 kinaweka utaratibu wa kumruhusu mwendesha ghala kuuza bidhaa kiasi chochote iwapo mwenye mali atashindwa kulipa tozo ya kuhifadhi mali yake ghalani.

Kamati inaona utaratibu huo wa kumwachia mwendesha ghala kujipangia kiasi cha tozo unaweza kutumika vibaya na hivyo Kamati inapendekeza Bodi ya Leseni ya Ghala ndiyo ipewe jukumu la kukadiria na kuidhinisha kiasi cha bidhaa kinachoweza kuuzwa kwa ajili ya kulipa gharama za utunzaji wa bidhaa ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 29 cha Muswada kinapendekeza viwango vya adhabu vinavyoweza kutolewa na Mahakama kuwa 150%. Kamati inaona viwango vya adhabu vinavyopendekezwa kutolewa na Mahakama ni vikubwa na havitekelezeki, hivyo Kamati inapendekeza viwango hivyo virekebishwe na kuwa 50%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 30 cha Muswada kinapendekeza viwango vya adhabu vinavyoweza kutolewa na Bodi kuwa 50%. Kamati inashauri viwango vya adhabu vinavyopendekezwa kutolewa na Bodi vya 50% ni vikubwa na havitekelezeki na inapendekeza viwango hivyo virekebishwe na kuwa 20%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 33 cha Muswada ambacho kinahusiana na adhabu hakijaweka kiwango cha chini cha adhabu, kwa msingi huo Kamati inapendekeza adhabu ya kiwango cha chini kuwa sio chini ya shilingi 5,000,000/= na haitazidi 10,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa jumla wa Kamati: Ili kuongeza ufanisi na urahisi wa utekelezaji wa marekebisho ya sheria inayopendekezwa, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla kama ifuatavyo:-

Ili Mfumo wa Stakabadhi wa Ghala uweze kuwa na tija inayokusudiwa, hauna budi kwenda sambamba na uanzishwaji wa Mfumo Rasmi wa Soko la Mazao ya Bidhaa *(Commodity Exchange)* kwa kuwa mabadiliko ya sheria inayopendekezwa yanaweka msingi wa kuwezesha utekelezaji wa mfumo wa soko la mazao na bidhaa kwa kuruhusu mazao yatakayohifadhiwa ghalani kuuzwa katika soko la mazao.

Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mchakato wa kuwa na sheria mahsusi ya mazao ya bidhaa uje kwa haraka.

Kwa kuwa, kilio kikuu cha wakulima wadogo ni kuwepo kwa gharama kubwa katika mfumo unaofanyiwa mabadiliko, Kamati inashauri mabadiliko ya sheria inayopendekezwa kuweka mfumo wa kuwagawa waweka mali katika makundi mawili, yaani kundi la msingi na kundi la pili. Kwa kufanya hivi wakulima wadogo wataweza kufaidika na utaratibu wa kuwa na maghala katika maeneo ya vijijini karibu na makazi yao na hivyo kukwepa gharama za usafirishaji wa mazao umbali mrefu.

Kamati inaitaka Serikali kutimiza wajibu wake kwa kuendeleza miundombinu ya barabara kutoka sehemu za uzalishaji hadi kwenye maghala ya kuhifadhia bidhaa. Barabara nyingi hazipitiki wakati wa mvua, maghala yaliyo mengi hayapo karibu na wakulima na yaliyo mengi hayajafikia kiwango kinachotakiwa kupata leseni ya kuhifadhia bidhaa na mengine yenye ubora hayatumiki ipasavyo.

Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kuwa kunakuwepo na maghala ya kutosha yanayoweza kuhifadhi pamoja na kuajiri watumishi wa kutosha watakaosaidia utendaji na ufuatiliaji wa viwango katika ngazi ya msingi.

Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha utungwaji wa kanuni mara baada ya utungwaji wa sheria hii na kuona umuhimu wa kushirikisha wadau kwenye zoezi la utungwaji wa kanuni.

Kamati pia inaishauri Serikali kuendelea na kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ili kuongeza uelewa kuhusu mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; Kwa niaba ya Kamati napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani kwa wadau wote walioshiriki katika kutoa maoni yao. Kamati inapenda kutoa pongezi zake za dhati kwa Wizara ya Viwanda na Biashara hususan Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dokta Abdallah Kigoda, Naibu Waziri Mheshimiwa Janeth Mbene, Katibu Mkuu Ndugu Uledi na watendaji wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa ushirikiano wao hadi kukamilika kwa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru wadau wote waliota michango yao kwa ajili ya kuboresha Muswada huu. Maoni na michango yao imesaidia Kamati kukamilisha utungwaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa michango na ushauri wao uliosaidia kuboresha marekebisho ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti ni Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula. Wajumbe wengine wa Kamati ni Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Aieshi K. Hilary, Mheshimiwa Ester Lukago Minza Midimu, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa David Zakaria Kafulila na Mheshimiwa Shawana B. Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajumbe wa Kamati wengine ni Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Vicky Pascal Kamata, Mheshimiwa Naomi Mwakyoma Kaihula, Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Engineer Habib J. Mnyaa, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga na Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kukushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyotuongoza.

Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashillilah na Watendaji wa Ofisi ya Bunge na Makatibu wa Kamati Ndugu Angella Shekifu na Ndugu Rachel Nyega na Msaidizi wa Kamati Ndugu Pauline Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, sasa namwita Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Mheshimiwa Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lao tukufu kutoa maoni kwenye Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi Ghalani kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) toleo la 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kigoma Kusini kwa kuendelea kuonesha ushirikiano mkubwa kwa dua na maombi hasa katika kipindi ambacho nilikuwa napita katika sakata gumu la *Escrow*.

Kwa nafasi ya pekee, napenda sana kumshukuru mke wangu kwa kuendelea kunipa moyo katika kutimiza majukumu yangu ya kifamilia, Jimbo na Taifa langu bila kujali nyakati ngumu za kisiasa tulizopita na ambazo tumeendelea kuzipitia kama familia. Naomba kuwahakikishia wakazi wa Kigoma Kusini na wananachi kwa ujumla kuwa bado nipo salama, nitaendelea kupambana na ufisadi wa Serikali hii kupitia UKAWA mpaka kieleweke. *(Makofi)*

Napenda kutoa pongezi kwa matokeo ya kihistoria yaliyotoa ushindi mkubwa kwa vyama vya UKAWA katika Uchaguzi wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji uliomalizika nchini. *(Makofi)*

Natoa pole kwa wanachama wote wa vyama vya *NCCR*, CHADEMA na *CUF* ambavyo vinaunda UKAWA ambavyo kwa njia moja ama nyingine wamepata majeraha mbalimbali kwenye miili yao na wengine wamebambikiziwa kesi na vyombo vya dola katika mchakato mzima wa kupambana katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji uliomalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kutoa pole kwa Watanzania wote waliopoteza maelfu ya ndugu zao na wapenzi wao katika mfululizo wa ajali za barabarani ambazo zinaendelea kila kukicha tangu mwisho wa mwaka jana.

Inasikitisha kwamba, wakati nchi inapita kwenye mfululizo wa ajali za barabarani Serikali ya CCM imeendelea kukaa kimya na kuona kama ni mpango wa Mungu ilihali ni udhaifu mkubwa wa Serikali na hususani Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Mathias Chikawe ambaye haonekani kuchukua hatua yoyote zaidi ya kuendelea kuzurura wakati roho za ndugu na jamaa na wapenzi wetu zinazidi kupukutika. Haya ndiyo madhara ya Mheshimiwa Rais kuendelea kulea Mawaziri mizigo aina ya Mathias Chikawe kwa gharama za roho za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni mfumo ambao unahusisha mweka mali, mwendesha ghala, mnunuzi na taasisi za fedha. Serikali Kuu na Serikali za Mitaa hushiriki katika kuratibu na kusimamia mfumo huu, wafanyabiashara na wasindikaji hupeleka mazao yao katika ghala ambayo mwendesha ghala huyapokea na baada ya kuyapima uzito na kuhakiki ubora mwendesha ghala hutoa stakabadhi ya ghala ambayo ni kielelezo cha kuonesha umiliki wa mazao husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu unaweza kutumika kwa ajili ya kumwezesha mweka mali kufanya biashara ikiwa ni pamoja na kupata mkopo kutoka katika taasisi za fedha au kuhifadhi kwa lengo la kupunguza uharibifu wa mazao au upotevu wa mazao baada ya kuvuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kabla ya kupitia baadhi ya vifungu ambavyo tunaona kama Kambi Rasmi ya Upinzani vinatakiwa kufanyiwa marejeo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa ufanisi wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani utasaidia sana ushindani wa bei ya mazao ya mkulima, ubora wa mazao yanayozalishwa, kuunganisha wakulima na watoa huduma wa fedha, kuongeza ajira katika kilimo na mazao pamoja na masoko na hivyo kuongeza mchango wa sekta hii muhimu ya kilimo kwenye uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani duniani kote ni maalum kwa ajili ya kusaidia masuala yafuatayo:-

Moja, kutoa bei ya ushindani kwa mwenye mazao, kuhakikisha kwamba wanunuzi wengi zaidi wanakuwepo na taarifa kwa wanunuzi na hivyo ushindani wa wanunuzi humsaidia mkulima.

Pili, ubora wa mazao kuongezeka kwa sababu wazalishaji nao watashindana katika ghala wakati wa manunuzi.

Tatu, kuunganisha wakulima na taasisi za fedha kwani stakabadhi inaweza kutumika kama dhamana ya kukopa.

Nne, inaongeza na kuimarisha mfumo wa kitaasisi na vyama vya ushirika ambavyo ndiyo msingi wa ujenzi wa uchumi vijijini ambako mafanikio yake yanategemea sana mifumo ya vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla:- Moja, ufisadi unavyokwamisha kuletwa kwa Sheria ya *Commodity Exchange Market*. Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na Wizara hii kuvuta miguu kwa miaka mingi kuleta Sheria ya *Commodity Exchange Market* ambao ndiyo mwarubaini wa tatizo la soko kwa mazao duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafahamika wazi kwamba tangu mwaka 2006 Serikali kupitia Wizara hii ilianza mchakato wa kuanzisha Mfumo wa Soko la Mazao kwa maana ya *Commodity Exchange Market* kama ilivyo kwenye nchi nyingine duniani ambapo wakulima wanafaidi jasho lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana kwamba tangu mwaka 2006 Wizara hii imeshindwa kukamilisha sheria ya kuandaa mfumo huo na badala yake inaleta sheria vipandevipande kwa majina ya Stakabadhi Ghalani badala ya kuleta sheria mama ambayo ndiyo msingi wa kutatua tatizo la masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ushahidi tosha kwamba wafanyabiashara wakubwa wa mazao wanafaidi jasho la wakulima kwa kulangua mazao yao kwa bei ya kutupa, ndiyo kikwazo cha kuletwa kwa Sheria ya *Commodity Exchange Market.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwa nchi kama Ethiopia iliyokuja Tanzania kujifunza namna ya kuanzisha Mfumo wa *Commodity Exchange Market* wakati Tanzania tukiwa katika hatua za awali, leo Ethiopia wameishakamilisha mfumo huo na sasa Wabunge tunakwenda kujifunza kwao namna ya mfumo huu wa soko unavyofanya kazi. Hii ni aibu sana kwa Serikali hii na ni kigezo tosha kwamba Serikali hii ya CCM inabeba wafanyabiashara wanyonyaji kwa gharama za umaskini wa wakulima. *(Makofi)*

Mbili, malipo ya wakulima na mawakala wa hifadhi ya chakula: Kumekuwepo na malalamiko ya wakulima na mawakala wa mazao ya chakula kutokana na kuiuzia Serikali mazao na kucheleweshewa malipo yao kwa muda mrefu. Utaratibu huu wa kuwakopa wakulima na kuchelewa kuwalipa unawafanya kwanza mawakala kushindwa kufanya biashara lakini pia unawapunja kutokana na kubadilika kwa thamani ya shilingi.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunapenda kujua, kwanza, nini msimamo wa Serikali juu ya madai ya mawakala wa wakulima ambao wameikopesha Serikali kwa muda mrefu na mpaka sasa hawajalipwa? Lakini pili, ni lini Serikali itaacha utaratibu wa kuwakopa mazao wakulima na badala yake inunue moja kwa moja?

Tatu, ufisadi usikwamishe maandalizi ya kanuni: Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuitaka Wizara ihakikishe kanuni za utekelezaji wa mabadiliko haya ya sheria zinakamilishwa haraka kwa sababu upo uzoefu wa Serikali kukaidi kuandika kanuni hasa pale Bunge linapopitisha sheria ambazo zipo kwa maslahi ya wananchi lakini zipo dhidi ya wafanyabiashara wa makampuni ambayo uadilifu wao una mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano ya ukaidi wa Serikali kutokuandika kanuni za kutekeleza sheria ambazo zinawabana wawekezaji na wafanyabiashara wasio waaminifu ni kukosekana mpaka leo Kanuni ya Sheria ya Madini ya 2010 *(Mining Act, 2010)* na Sheria ya Mawasiliano *(Telecom Act, 2010)* ambazo kwa kuwa zililenga kuyabana makampuni na migodi, kuorodhesha hisa zake kwenye Soko la Mitaji ili kwanza, Watanzania wawe ni sehemu ya wamiliki, lakini, pili hesabu za Makampuni hayo na migodi hiyo ziwe wazi na hivyo Serikali iweze kupata kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizo mpaka leo kanuni zake zimekwama kwa sababu kampuni za simu na migodi wamegoma. Katika mazingira kama haya Kambi Rasmi ya Upinzani tukisema Serikali hii imewekwa mfukoni na wanyonyaji ambao ni migodi na kampuni za simu, wanaonyonya jasho la Watanzania, Serikali hii inapataje uhalali wa kupinga hoja hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa Wizara hii ni lazima iseme hapa Bungeni ni lini itakamilisha kanuni za sheria hii ili tusikutane na maajabu ya sheria hizo hapo juu ambazo Mawaziri wake bado wanazurura kila siku zaidi ya miaka mitano bila kuandaa kanuni ambazo zingesaidia kuongeza mapato katika bajeti ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu huu wa Serikali hii upo uwezekano kabisa kwamba kanuni za mabadiliko ya sheria hii zitakamilika ndani ya Serikali ya awamu ya sita kama CCM itaruhusiwa kuendelea kutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiukwaji wa sheria katika usimamizi wa mfumo: Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani umekuwa ukilalamikiwa sana na wakulima kwa sababu zifuatazo:-

Moja, wakulima wanalazimishwa kutumia vyama vya msingi na ushirika kama sharti la kutumia ghala wakati sheria haisemi hivyo. Ni vema ieleweke kuwa mkulima anapotumia ushirika analazimika kukatwa gharama ambazo angeweza kuziepuka. Kwa mfano, kwa kutumia ushirika, mkulima analazimika kulipa riba ya mkopo ambao shirika umechukua, analazimika kulipa gharama za uendeshaji wa chama cha msingi, analazimika kulipa gharama za ushirika ambazo zingekuwa siyo za lazima kama mkulima asingeamua kutumia ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya yanatokana na upungufu wa uendeshaji, siyo sheria na ni wazi kwamba upungufu huu unatokana na Waziri kwa kushirikiana na Bodi mbalimbali na mtandao mzima wa wanaoitwa wadau hasa kwenye zao la korosho kushindwa kusimamia sheria kwa maslahi wanayoyapata kwa kushirikiana na vigogo wafanyabiashara wanaofaidi jasho la wakulima wengi maskini kabisa. Kwani haiingii akilini vyama vya msingi na ushirika kudhibiti wakulima kwa maslahi ya viongozi hao wa vyama, Waziri na Waziri kubaki anafumbia macho kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria haisemi kwamba ni lazima tu apitie chama cha msingi, lakini Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla wameendelea ku-*collude* na Vyama vya Msingi, Ushirika na Bodi kulazimisha wakulima wapitie ushirika, kitu ambacho kwenye sheria hakipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa upangaji bei: Utaratibu mzima wa upangaji bei *(bei dira)* kwa kiasi kikubwa unaamuliwa kwa njama za wanunuzi, vigogo wa Serikali na viongozi wa Bodi ya Ushirika, Bodi ni tatizo. Ndiyo maana siku zote wakulima wamekuwa wakitaka kuuza mazao yao nje ya mfumo huu kwa sababu wanataka wapate bei nzuri. Leseni za ununuzi zinatolewa kwa makampuni teule ambayo karibu ni yaleyale miaka nenda miaka rudi, hakuna ushindani.

Sita, kuuza mazao ghafi baada ya kuuzwa viwanda: Lengo kubwa la sheria zote hizi ni kuongeza thamani ya mazao na ubora wa bei kwa mkulima. Mfumo wa Stakabadhi Ghalani lengo lake ni kumsaidia mkulima kupata bei nzuri, duniani kote. Huwezi kupata bei nzuri kwa kuuza mazao ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mheshimiwa Waziri Kigoda katika Awamu ya Tatu ndiye aliyesimamia ubinafsishaji wa viwanda kwa kuviuza kwa bei ya kutupa. Mfano rahisi ni viwanda 12 vilivyouzwa kwa wawekaji matapeli walioshindwa kuvifufua na sasa wakulima wanapata bei duni kwa kuuza korosho ghafi ambayo bei yake ni ya chini mno sawa sawa na unyonyaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatamka kuwa Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla wawaeleze Watanzania ni lini Serikali itarejesha viwanda hivi vya korosho kwa matapeli hao na vingine ambavyo kwa ujumla matapeli walipewa kwa jina la wawekezaji, wameshindwa kuviendeleza na kuvigeuza kuwa magofu na maghala ya kuhifadhia vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu maalum: Marekebisho yanayofanywa kwenye kifungu cha 6(4)(b) kinachoongeza vifungu vya (2), (3), na (4) kwa mujibu wa kifungu cha 6(a) cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya 2005, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977.

Mheshimkiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa anatekeleza:- Na-*quote*;

"Kuingilia kati katika hatua yoyote ya mashauri yoyote, rufaa yoyote, kukaza hukumu yoyote au katika mashauri yanayohusiana nayo katika Mahakama yoyote au Baraza lolote ambapo haki ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imezuiliwa na Sheria".

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Mashauri, Sura ya 5 ya sheria ya Tanzania, ijapokuwa ni kweli kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha sheria hiyo kwamba Serikali na watumishi wake wanaweza kushitakiwa kwa makosa mbalimbali wanayoyatenda wakati wakitimiza majukumu yao kama watumishi wa Serikali, masharti yaliyopo katika sheria hiyo yamefanya utekelezaji wa haki ya kuishitaki Serikali au watumishi kuwa ngumu mno sawa sawa na haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa mujibu wa kifungu cha 6(2); mtu yeyote anayekusudia kufungua mashauri dhidi ya Serikali, ni lazima kwanza awasilishe kusudio hilo kwa Waziri wa Serikali, idara au afisa anayehusika kwa *notice* ya muda usiopungua siku 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kinamlazimu mdai kueleza misingi na madai dhidi ya Serikali na ni lazima apeleke nakala ya *notice* kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Bila kutimiza masharti haya kifungu cha 4(2) kinasema wazi kwamba hakuna shauri litakalofunguliwa dhidi ya Serikali na kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawakili na wadau wengi waliokumbana na makali na masharti haya wanafahamu jinsi ambavyo kesi nyingi dhidi ya Serikali hutupiliwa mbali na Mahakama zetu kila mwaka na hivyo wananchi wengi wanaumizwa na Serikali hii au watendaji au watumishi kukosa haki zao kwa sababu tu ya kutimizwa kwa masharti magumu ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 5 kinachoingiza kifungu kipya kwenye sheria ya kutoa *license of collateral managers;* kwa bahati mbaya maneno hayo hayakutolewa tafsiri katika sheria yoyote kwenye Muswada. Hoja nyingine ni kuwa, hao *collateral managers* watakuwa wanawajibika kwa mamlaka ipi? Wamewekwa lakini hakuna utaratibu wa uwajibikaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6 kinachofanyia marekebisho Kifungu cha 6 cha Sheria Mama, kinaoongeza kifungu kipya cha 3 (a) na (b). Kifungu cha (b) kinachosema kuwa, Kamati za Mikoa na Wilaya zitasimamiwa chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya.

Wakizungumza katika Mkutano Mkuu wa 13 wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya hizo *(MAMCU)*, uliofanyika Agosti, 2012 Mjini Masasi, Viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika wa Kilimo na Masoko vya Wilaya ya Mtwara, Masasi na Nanyumbu, Mkoani Mtwara, vimetishia kujiondoa katika Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, unaotumika katika ununuzi wa Zao la Korosho kwa madai kuwa umekuwa tishio kwa mali na usalama wao iwapo Viongozi wa Kisiasa kama Wakuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wataendelea kuingilia utekelezaji wa kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viongozi au Makada hao wa Chama, waliweza kuingilia utaratibu bila ya uwepo wa sheria za kuwaruhusu. Je, kama sheria ikiwapa ruhusa ni nini kitatokea?

Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Kifungu cha 3(b) kifutwe rasmi. Aidha, Kifungu cha 3(a) kinachozitaka mamlaka za Mikoa na Wilaya kuunda Kamati za usimamizi wa mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani, Kambi Rasmi ya Upinzani inaungana na wadau ambao walitaka kufahamu gharama za uendeshaji wa Kamati hizo zitatoka wapi. Je, ni kwenye Bodi ya Korosho au kwenye Bajeti ya Halmashauri za Wilaya ambazo zinazalisha Zao hilo la Korosho au mazao mengine au mzigo wa kuendesha Kamati hizo utatolewa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 20 cha Muswada kinachofanya mabadiliko kwenye Kifungu cha 38 cha Sheria Mama kwa kufuta kifungu kidogo cha kwanza (1) na kuweka kingine kinachosomeka kwamba: " *(1) The holder shall, in the case of loss, theft or destructions of warehouse receipt, immediately report to warehouse operator or collateral manager, as the case may be.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba, kwa kuwa kuna suala la upotevu, wizi na uharibifu wa mali, basi hilo ni suala la jinai na *in case* likiwepo ni suala la kupelekwa Polisi na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 28(2) na (3) cha Muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 60 cha Sheria Mama kinasomeka kwamba; "*(2)-where a warehouse operator refuses to deliver goods for the purpose of satisfying a lien, the Board may apply to court to sell the goods*".

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki kinajichanganya, kwani dhana nzima ya utaratibu huu au mfumo mzima ni kuwa mtunza au mwendesha ghala si mmiliki wa mali zilizomo kwenye ghala, hivyo yeye hawezi kuuza mali hizo hadi pale zitakapouzwa na mkulima au mmiliki wa mali zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hoja ya pili ni kwamba, mtunza ghala au mwendeshaji ghala ndiye anayestahiki kuuza mali ili kujilipa kutokana na ukweli kwamba, ndiye mdau anayeweza kuingia kwenye madeni na siyo vinginevyo. Kwa ukweli huo, Bodi haina msingi wa kuomba amri ya mahakama kuuza bidhaa zilizomo kwenye ghala. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka vifungu hivi vifutwe kwani havina maana yoyote zaidi ya kuleta urasimu usio wa lazima na mkanganyiko wa kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kusisitiza kwamba, mabadiliko ya sheria yaliyoletwa ni mengi mno kiasi ambacho ni sawa na kuandika sheria upya. Zaidi ni vema ikaeleweka kwamba, malalamiko ya wakulima na wazalishaji wanaotumia mfumo wa stakabadhi ghalani, hayakuhusu sana upungufu wa kisheria bali utendaji mbovu, uozo na ufisadi mkubwa katika usimamizi wa mfumo mzima kuanzia ngazi ya Bodi mpaka Serikalini. *(Makofi)*

Serikali inatoa vibali kwa mfano, kwa wafanyabiashara kuingiza mazao kama mchele kinyemela bila kodi. Mchele unaingizwa nchini bila kodi na kushindanishwa na mchele wa ndani ambao umehifadhiwa kwenye maghala. Kwa upande mmoja wakulima wanaumia kwa kushindwa kushindana, lakini zaidi Serikali inapoteza mabilioni ya kodi kutokana na uingizaji huo wa mchele na mazao mengine ambayo vibali vyake vinatolewa kinyemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika msingi huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuisisitizia Serikali kuchukua hatua kuhusu uozo katika utendaji katika maeneo hayo hasa utoaji na uingizaji wa mazao kinyemela bila kodi. Serikali na Mawaziri wote wanajua ukubwa wa tatizo hili. Vibali vinatolewa kinyemela vya kuingiza mazao kwa hoja kwamba, kuna tatizo la chakula. Bahati mbaya sana hata ambapo hakuna tatizo la chakula, vibali vinatolewa kinyemela. Lazima Vyombo ya Usalama hususan Polisi, vijielekeze kwenye kusimamia na kudhibiti uingizwaji huu wa bidhaa kutoka nje kwa njia za bandari bubu, badala ya kutumia muda mwingi kupambana na vijana wajasiriamali kwa jina la bodaboda huku masuala ya msingi yanayogusa uchumi kama haya wakiyatazama na kuyaacha yaendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Bagamoyo mpaka Bandari ya Dar es Salaam ni kilomita 70, lakini kuna Bandari Bubu 32! Utaona ni kwa namna gani ambavyo Serikali hii imeshindwa kudhibiti nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara ya Viwanda na Biashara Kama Ilivyowasilishwa Mezani**

**MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI- WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA MHE. DAVID ZACHARIA KAFULILA (MB) KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MFUMO WA STAKABADHI GHALANI YA MWAKA 2013**

*"The warehouse Receipts (Amendments) Act, 2013*

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa maoni kwenye Muswada huu wa marekebisho ya sheria ya mfumo wa stakabadhi Gharani kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mujibu wa kanuni za Bunge, kanuni ya 86(6) toleo la mwaka 2013.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wote wa jimbo la Kigoma kusini kwa kuendelea kuonesha ushirikiano kwa dua na maombi yao kwangu nikiwa kwenye kipindi kigumu cha mapambano ya kusimamia uwajibikaji wa serikali hasa katika sakata la escrow ambalo kwa hakika ukaribu wao uliongeza ujasiri wangu.

Kwa nafasi ya pekee namshukuru sana mke wangu kwa kuendelea kunipa moyo katika kutimiza majukumu yangu kwa jimbo na taifa langu bila kujali nyakati ngumu za siasa tulizopita na ambazo tumeendelea kuzipitia kama familia. Naomba kuwahikishia wakazi wa Kigoma Kusini na wananchi kwa ujumla kuwa bado nipo salama, tutaendelea kupambana na ufisadi wa serikali hii kupitia UKAWA mpaka kieleweke.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa pongezi kwa matokeo ya kihistoria yalitoa ushindi mkubwa kwa vyama vya UKAWA katika uchaguzi wa vijiji, mitaa na vitongoji uliomalizika nchini.

Natoa pole kwa wanachama wote wa vyama vinavyounda UKAWA ambao kwa njia moja ama nyingine wamepata majeraha mbalimbali kwenye miili yao na wengine

wamebambikizwa kesi na vyombo vya dola katika mchakato mzima wa uchaguzi wa Serikali za mitaa, vijiji na vitongoji uliomalizika.

**Mheshimiwa Spika,** aidha napenda kutoa pole kwa watanzania wote waliopoteza maelfu ya ndugu zao katika mfululizo wa ajali za barabarani ambazo zinaendelea kila kukicha tangu mwisho wa mwaka jana. Inasikitisha kwamba wakati nchi inapita kwenye mfululizo wa ajali za barabarani, Serikali ya CCM imeendelea kukaa kimya na kuona kama ni mpango wa Mungu ilhali ni udhaifu mkubwa wa Waziri wa Mambo ya Ndani, Bw. Chikawe, ambaye haonekani kuchukua hatua yoyote zaidi ya kuendelea kuzurura wakati roho za ndugu na wapenzi wetu zinazidi kupukutika. Haya ndio madhara ya Mheshimiwa Rais kuendelea kulea Mawaziri mizigo aina ya Mathias Chikawe kwa gharama ya roho za Watanzania.

**Mheshimiwa Spika,** mfumo wa stakabadhi ghalani ni mfumo unaowahusisha mweka mali, Mwendesha ghala, mnunuzi na taasisi za fedha. Serikali Kuu na Serikali za Mitaa hushiriki katika kuratibu na kusimamia mfumo huu.Wafanyabiashara na wasindikaji hupeleka mazao yao katika ghala ambayo mwendesha ghala huyapokea baada ya kuyapima uzito na kuhakiki ubora. Mwendesha ghala hutoa stakabadhi ya ghala ambayo ni kielelezo cha kuonesha umiliki wa mazao husika.

**Mheshimiwa Spika,** mfumo huu unaweza kutumika kwaajili ya kuwezesha mweka mali kufanya biashara ikiwa ni pamoja na kupata mkopo toka taasisi za fedha au kuhifadhi kwa lengo la kupunguza uharibifu wa mazao au upotevu wa mazao baada ya kuvuna.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa utangulizi huo, na kabla ya kupitia baadhi ya vifungu ambavyo tunaona vinatakiwa kufanyiwa marejeo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa ufanisi wa mfumo wa stakabadhi ghalani utasaidia sana ushindani wa bei ya mazao ya mkulima, ubora wa mazao yanayozalishwa, kuunganisha wakulima na huduma za fedha, kuongeza ajira katika kilimo na masoko, na hivyo kuongeza mchango wa sekta hii muhimu kwa uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa Stakabadhi ghalani duniani kote ni maalumu kwa ajili ya kusaidia masuala yafuatayo:-

(I) Kutoa bei ya ushindani kwa mwenye mazao. Kwa kuhakikisha wanunuzi wengi zaidi wanakuwa na taarifa na hivyo kushindana katika bei hali ambayo inamsaidia mkulima kupata bei bora zaidi.

(II) Ubora wa mazao kuongezeka kwasababu ya ushindani wa mazao kwenye ghala yaliyowekwa na wakulima mbalimbali.

(III) Kuunganisha wakulima na taasisi za fedha, kwani stakabadhi inaweza kutumika kama dhamana ya kukopa.

(IV) Inaongeza na kuimarisha mifumo ya kitaasisi na vyama vya ushirika ambavyo ndio msingi wa ujenzi wa uchumi vijijini ambako mafanikio yake yanategemea sana mifumo ya vyama vya ushirika.

**MAONI YA JUMLA**

**1. Ufisadi ulivyokwamisha mfumo wa Commodity Exchange Market**

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na Wizara hii kuvuta miguu kwa miaka mingi kuleta sheria ya soko la mazao (Commodity Exchange Market) ambayo ndio mwarobani kwa tatizo la soko la mazao kama ilivyo katika nchi nyingi duniani.

**Mheshimiwa Spika,** inafahamika wazi kuwa tangu mwaka 2006 Serikali kupitia wizara hii ilianza mchakato wa kuanzisha mfumo wa soko la mazao kama ilivyo kwenye nchi nyingi duniani ambako wakulima wanafaidi jasho lao.

**Mheshimiwa Spika,** ni bahati mbaya sana kwamba tangu mwaka huo 2006, wizara imeshindwa kukamilisha sheria ya kuandaa mfumo huo na badala yake inaleta sheria vipande vipande vya stakabadhi ghalani badala ya kuleta sheria mama ya mfumo wa soko la mazao (Commodity Exchange Market).

**Mheshimiwa Spika,** huu ni ushahidi tosha kwamba wafanyabiashara wakubwa wanaofaidi jasho la wakulima kwa kulangua mazao yao kwa bei ya kutupa ndio kikwazo cha kuletwa sheria ya commodity exchange market.

**Mheshimiwa Spika,** ni aibu kwa nchi kama Ethiopia ilikuja Tanzania kujifunza namna ya kuanzisha mfumo wa commodity exchange market, wakati Tanzania tukiwa katika hatua za awali, leo Ethiopia wameshakamilisha mfumo huu na sasa tunaenda kujifunza kwao namna mfumo huu wa soko unavyofanya kazi. Hii ni aibu sana kwa serikali na ni kielelezo tosha kwamba serikali ya CCM inabeba wafanyabiashara wanyonyaji kwa gharama za umasikini wa wakulima.

**2. Malipo kwa Wakulima na Mawakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (National Food Reserve Agency-NFRA).**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na malalamiko ya wakulima na mawakala wa mazao ya chakula kutokana na kuiuzia serikali mazao na kucheleweshewa malipo yao kwa muda mrefu, utaratibu wa kuwakopa wakulima na kuchelewesha kulipa unawafanya kwanza mawakala kushindwa kufanya biashara na pia kuwapunja kutokana na kubadilika kwa thamani ya shilingi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kujua:-

(a) Kwanza nini msimamo wa serikali juu ya madai ya mawakala na wakulima ambao wameikopesha serikali kwa muda mrefu na mpaka sasa hawajalipwa?

(b) Pili ni lini serikali itaacha kuwakopa wakulima mazao yao na kununua na kufanya malipo papo hapo?

(c) Tatu je serikali itakua tayari kulipa riba ya madeni ambayo wakulima na mawakala wa mazao ya chakula wamekua wakiwadai? Kwani ni wazi hata mawakala pia wanakopa benki ili kuweza kuwa na mitaji ya kufanya biashara na wanawajibika kulipa riba katika mabenki?

**3. Ufisadi usikwamishe maandalizi ya kanuni**

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuitaka wizara ihakikishe kanuni za utekelezaji wa mabadiliko haya ya sheria zinakamilishwa haraka kwa sababu upo uzoefu wa

serikali hii kukaidi kuandika kanuni hasa pale Bunge linapopitisha sheria zinazokwaza maslahi ya wafanyabiashara na wawekezaji wasio waaminifu**.**

**Mheshimiwa Spika,** mifano ya ukaidi wa serikali kutokuandika kanuni za kutekeleza sheria zinazobana wawekezaji na wafanyabiashara wasio waaminifu ni kukosekana mpaka leo kanuni za sheria ya madini ya 2010 (Mining Act 2010) na sheria ya mawasiliano ya 2010 (Telecom & Postal Act 2010) ambazo kwa kuwa zililenga kuyabana makampuni ya simu na migodi kwa kuhakikisha yanaorodhesha hisa zake kwenye soko la mitaji ili:-

(a) Watanzania wawe sehemu ya wamiliki; na

(b) Hesabu za kampuni husika kuwa wazi ili serikali ipate kodi sahihi.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hizo mpaka leo Kanuni zake zimekwama kwa sababu kampuni za simu na migodi imegoma. Katika mazingira haya Kambi Rasmi ya Upinzani tukisema serikali imewekwa mfukoni na mafisadi wanaonyonya jasho la Watanzania, serikali ina inapataje uhalali wa kupinga?

**Mheshimiwa Spika,** ndio sababu Kambi Rasmi ya Upinzani tunasisitiza hapa kuwa Wizara hii lazma iseme hapa bungeni ni lini itakamilisha kanuni za sheria hii ili tusikutane na maajabu ya sheria hizo hapo juu ambazo mawaziri wake bado wanazunguka kila siku kwa zaidi ya, miaka mitano bila kuandaa kanuni ambazo zingesaidia kuongeza mapato ya nchi kwa kiasi kikubwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uzoefu huu wa serikali hii, upo uwezekano wa kanuni za mabadiliko ya sheria hii kukamilika ndani ya serikali ya awamu ya sita kama CCM itaachwa iendelee kutawala nchi hii.

**4. Ukiukwaji wa sheria katika usimamizi wa mfumo**

**Mheshimiwa Spika,** usimamizi wa mfumo wa stakabadhi ghalani umekuwa ukilalamikiwa sana na wakulima kwa sababu zifuatazo:-

I. Wakulima wanalazimishwa kutumia vyama vya msingi vya ushirika kama sharti la kutumia ghala wakati sheria haisemi hivyo. Ni vema ieleweke kuwa mkulima anapotumia ushirika analazimika kukatwa gharama ambazo angeweza kuepuka. Kwa mfano kwa kutumia ushirika mkulima analazimika kulipa riba ya mkopo anaochukua, analazimika kulipa gharama za uendeshaji wa chama cha msingi, kulipa gharama za Ushirika, gharama ambazo zingekuwa lazima kwa mkulima ambaye sio mwanachama.

**Mheshimiwa Spika,** matatizo haya yanatokana na mapungufu ya uendeshaji, sio ya kisheria. Na ni wazi kwamba mapungufu haya yanatokana na waziri kwa kushirikiana na bodi na mtandao mzima wa wanaoitwa wadau hasa kwenye zao la korosho kushindwa kusimamia sheria kwa maslahi anayoyapata yeye kwa kushirikiana na vigogo wenzake wanaofaidi jasho la wakulima wengi masikini kabisa, Kwani haingiii akilini vyama vya msingi na ushirika kudhibiti wakulima kwa maslahi ya viongozi hao wa vyama na waziri kufumbia macho kinyume cha sheria.

**5. Utaratibu wa upangaji bei dira**

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu mzima wa upangaji wa bei dira kwa kiasi kikubwa unaamuliwa kwa njama za wanunuzi, vigogo wa serikali na viongozi wa bodi na Ushirika. Ndio maana siku zote wakulima wamekuwa wakitaka kuuza mazao yao nje ya mfumo huu kwa

sababu wapate bei nzuri zaidi. Leseni za ununuzi zinatolewa kwa makampuni teule ambayo ni yale yale kwa miaka zaidi ya kumi.

**6. Kuuza mazao ghafi baada ya kuua viwanda**

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa stakabadhi gahalani lengo lake ni kusaidia mkulima kupata bei nzuri. Lakini duniani kote, huwezi kupata bei nzuri kwa kuuza mazao ghafi. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri Kigoda katika awamu ya tatu ndiye aliyesimamia ubinafsishaji wa viwanda kwa kuviuza bei ya kutupa.

**Mheshimiwa Spika,** mfano rahisi ni viwanda vya korosho 12 vilivyobinafsishwa kwa wawekezaji matapeli, wameshindwa kuvifufua na sasa wakulima wanapata bei duni kwa kuuza korosho ghafi ambayo bei yake ni chini mno.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi rasmi ya upinzani inamtaka Mhe Waziri Kigoda na serikali kwa ujumla aeleze watanzania ni lini serikali itarejesha viwanda hivi vya korosho na vingine ambavyo kwa ujumla ambavyo matapeli waliopewa kwa jina la wawekezaji wameshindwa kuviendeleza na kuvigeuza magofu ya kuhifadhiwa au karakana.

**VIFUNGU MAALUMU**

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho yanayofanywa kwenye kifungu cha 4(b) kinachoongeza vifungu vipya vya 2, 3 na 4.

Kwa mujibu wa kifungu cha 6(a) cha *Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya 2005*, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa ibara ya 59(3) ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977*.

Mwanasheria Mkuu atakuwa na atatekeleza mamlaka ya "... *kuingilia kati katika hatua yoyote ya mashauri yoyote, rufaa yoyote, kukaza hukumu yoyote au katika mashauri yanayohusiana nayo katika mahakama yoyote au baraza lolote ambapo haki ya Mwanasheria Mkuu kusikilizwa imezuiliwa na sheria.*"

**Mheshimiwa Spika,** katika *Sheria ya Mashauri ya Serikali, Sura ya 5 ya Sheria za Tanzania*. Ijapokuwa ni kweli, kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria hiyo, kwamba Serikali na watumishi wake mbali mbali wanaweza kushtakiwa kwa makosa mbali mbali wanayoyatenda wakati wakitimiza majukumu yao kama watumishi wa Serikali, masharti yaliyopo katika Sheria hiyo yamefanya utekelezaji wa haki ya kuishtaki Serikali au watumishi wake kuwa ngumu mno.

**Mheshimiwa Spika,** kwanza, kwa mujibu wa kifungu cha 6(2), mtu yeyote anayekusudia kufungua mashauri dhidi ya Serikali lazima kwanza awasilishe kusudio hilo kwa Waziri wa Serikali, Idara au ofisa anayehusika kwa notisi ya muda usiopungua siku tisini. Kifungu hicho kinamlazimu mdai huyo kuelezea msingi wa madai yake dhidi ya Serikali na lazima apeleke nakala ya notisi hiyo kwa Mwanasheria Mkuu. Bila kutimiza masharti haya, kifungu cha 6(2) kinasema wazi kwamba "*hakuna shauri litakalofunguliwa dhidi ya Serikali na kusikilizwa....*"

**Mheshimiwa Spika,** Mawakili na wadau wengi waliokumbana na makali ya masharti haya wanafahamu jinsi ambavyo kesi nyingi dhidi ya Serikali hutupiliwa mbali na mahakama zetu kila mwaka – na hivyo wananchi wengi walioumizwa na Serikali hii au na watendaji na watumishi wake kukosa haki zao - kwa sababu tu ya kutotimizwa kwa masharti ya kifungu cha 6(2) cha Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** pili, kwa mujibu wa kifungu cha 6(4) cha Sheria ya Mashauri ya Serikali, "*mashauri yote dhidi ya Serikali yatafunguliwa katika Mahakama Kuu....*"

Hivyo basi, kwa ukweli huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta vifungu hivyo kwani vina lengo la kuwanyima watu haki zao za msingi. Ikichukuliwa maanani kuwa, kwa mujibu wa kifungu cha 4 (2) cha sheria mama kuwa bodi ni chombo chenye mamlaka kamili na hivyo kuwa na uwezo wa kushtaki na kushtakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 5 kinachoingiza kifungu kipya kwenye sheria cha *(b) licensing of collateral managers.* Kwa bahati mbaya maneno hayo hayakutolewa tafsiri yoyote kwenye muswada na pia hoja nyingine ni kuwa hao collateral managers watakuwa wanawajibika kwa mamlaka ipi?

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 kinachofanyia marekebisha kifungu cha 6 cha sheria mama kinachoongeza kifungu kipya cha 3 (a) na (b). Kifungu cha (b) kinachosema kuwa kamati za mikoa na wilaya zitasimamiwa chini ya uenyekiti wa Mkuu na Mkoa na Mkuu wa Wilaya.

**Mheshimiwa Spika,** wakizungumza katika mkutano mkuu wa 13 wa chama kikuu cha ushirika cha wilaya hizo (Mamcu) uliofanyika August,2012 mjini Masasi, viongozi wa VYAMA vya Msingi vya Ushirika wa Kilimo na Masoko vya wilaya ya Mtwara, Masasi na Nanyumbu mkoani Mtwara vimetishia kujiondoa katika mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani unaotumika katika ununuzi wa zao la Korosho kwa madai umekuwa tishio kwa mali na usalama wao iwapo viongozi wa kisiasa na serikali wataendelea kuingilia utendaji kazi wao.

**Mheshimiwa Spika,** Viongozi hao au makada hao wa chama waliweza kuingilia utaratibu bila ya uwepo wa sheria ya kuwaruhusu, je kama sheria ikiwapa ruhusa rasmi ni nini kitatokea? Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kifungu hiki cha 3(b) kifutwe rasmi.

Aidha, kifungu cha 3(a) kinachozitaka mamlaka za mikoa na Wilaya kuunda Kamati za usimamizi wa mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani, Kambi Rasmi ya Upinzani inaungana na wadau ambao walitaka kufahamu gharama za uendeshaji wa kamati hizo zitatoka wapi? Je ni kwenye Bodi ya Korosho au kwenye bajeti ya halmashauri za Wilaya ambazo zinazalisha zao hilo la Korosho. Au mzigo wa kuendesha kamati hizo utaelekezwa kwa wakulima wenyewe, jambo ambalo halitokubalika kwa njia yoyote ile.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya kuwa na Sheria ya "Commodity Exchange Market" Kanuni za utekelezaji wa sheria hii kifungu cha 5(1) na (2) kinaeleza yafuatayo, nanukuu: "(1) In executing its functions pursuant to section5 of the Act and Regulation 4 of these regulations, the Board shall be required to establish or facilitate the establishment of the market mechanisms frameworks and networks that shall ensure increasing involvement of many commodities in the warehouse receipt system. (2) Mechanisms for increasing involvement of commodities in the warehouse receipt system may include, but not limited to the establishment of a commodity Exchange Market."

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 20 cha muswada kinachofanya mabadiliko kwenye kifungu cha 38 cha sheria mama kwa kufuta kifungu kidogo cha 1 na kuweka kingine kinachosomeka kwamba: *" (1) The holder shall, in the case of loss, theft or destruction of a warehouse receipt, immediately report to warehouse operator or collateral manager, as the case may be,"*

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kwa kuwa kuna suala la upotevu, wizi na uharibifu wa mali basi hilo ni suala la jinai na likishakuwepo suala la jinai sehemu mwafaka kutoa taarifa ni polisi na baadae ndipo taarifa itolewe kwa mujibu wa kifungu hiki.

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kifungu hiki kirekebishwe ili taarifa kwanza itolewe polisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 26 kifungu kidogo cha (2) na (3) cha muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 60 cha sheria mama. Kinachosomeka kuwa:

> *"(2)-where a warehouse operator refuses to deliver goods for the purpose of satisfying a lien, the Board may apply to court to sell the goods".*

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki kinajichanganya kwani dhana nzima ya utaratibu huu au mfumo mzima ni kuwa mtunza/mwendesha ghala si mmiliki wa mali zilizomo kwenye ghala hivyo yeye hawezi kuuza mali hizo hadi pale zitakapouzwa na mkulima au mmiliki kupatiwa stahili zake.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, hoja ya pili ni kwamba mtunza ghala au mwendeshaji ghala ndiye anayestahili kuuza mali ili kujilipa kutokana na ukweli kwamba ndiye mdau anayeweza kuingia kwenye madeni na sio mdau mwingine yeyote. Hivyo basi, kwa ukweli huo bodi haina msingi wa kuomba amri ya mahakama kuuza bidhaa zilizomo kwenye ghala.

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka vifungu hivi vifutwe kwani havina maana yoyote zaidi ya kuleta mkanganyiko kiutendaji.

**MWISHO**

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kusisitiza kwamba, mabadiliko ya sheria yaliyoletwa ni mengi mno kiasi ni sawa na kuandika upya sheria yenyewe. Lakini zaidi ni vema ikaeleweka kwamba malalamiko ya wakulima na wazalishaji wanaotumia mfumo huu wa stakabadhi ghalani hayakuhusu mapungufu ya kisheria bali utendaji mbovu na uozo na ufisadi mkubwa katika usimamizi wa mfumo mzima wa soko.

Serikali inatoa vibali kwa wafanyabiashara kuingiza mazao kama mchele kinyemela bila kodi. Mchele unaingizwa nchini bila kodi na kushindanishwa na mchele unaozalishwa nchini. Kwa upande mmoja wakulima wanaumia kwa kushindwa kushindana lakini zaidi serikali inapoteza mabilioni ya shilingi kutokana na ukwepaji kodi unaofanywa kupitia vibali vinavyotolewa kinyemela, bandari bubu na mfumo mzima wa kifisadi katika bandari ya Dar es salaam.

**Mheshimiwa Spika,** ni katika msingi huo, Kambi rasmi ya upinzani inapenda kusisitiza serikali kuchukua hatua kuhusu uozo katika utendaji katika maeneo hayo hasa ya utoaji na uingizaji wa mazao kinyemela bila kodi. Serikali na mawaziri wote wanajua ukubwa wa tatizo hili. Ni lazima vyombo ya usalama hususan polisi ijielekeze kwenye kusimamia na kudhibiti uingizwaji huu wa bidhaa kutoka nje kwa njia ya bandari bubu badala ya kutumia muda mwingi kupambana na vijana wajasiriamali kama bodaboda huku masuala ya msingi kama haya yanawashinda.

Naomba kuwasilisha.

**David Z. Kafulila (MB)**
**Waziri Kivuli Viwanda na Biashara**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, ninamshukuru Waziri na Wenyeviti. Wachangiaji wa leo ni wachache sana na kwa vile Muswada huu unatakiwa uishe muda huu, kwa hiyo, tunatoa nafasi kwa watu wanne na watachangia hao hao. Tunaanza sasa na Mheshimiwa Said Arfi, wajiandae Mheshimiwa Mtutura, Mheshimiwa Salum Barwany na Mheshimiwa David Kafulila. Mheshimiwa Said Arfi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya awali ya kuchangia katika Muswada ulio mbele yetu. Muswada huu unalenga kumsaidia nani? Kama lengo ni kumsaidia mkulima mdogo maskini, Muswada huu haumsaidii huyu mkulima ambaye ndiye anayezalisha chakula katika nchi yetu. Muswada huu ni mzigo tu kwa mkulima ambaye atabeba gharama za utunzaji na uhifadhi wa mazao yake katika maghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya mkulima huyu ni kuuza mazao yake, halimi kwa ajili ya kwenda kuweka mazao katika ghala. Analima ili auze mazao aweze kujikimu, apate matumizi ya familia yake, aweze kulipa michango ya Serikali inayotozwa ya kujenga maabara na kadhalika kutokana na mazao anayoyazalisha. Matokeo yake mkulima huyu analazimishwa kwenda kuweka mazao yake ghalani bila soko kufahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni soko la mazao. Nilikuwa ninapata shida sana na ninajiuliza mara zote kwamba, je, mazao yameondolewa katika mfumo wa soko huria? Kama yameondolewa katika mfuko wa soko huria ni nani sasa ananunua mazao? Je, hao wanunuzi wa mazao wanatambulika, wanalipa kodi au kila mtu mwenye uwezo wa kununua magunia tano au sita basi anaweza kuwa ni mnunuzi wa mazao? Eneo hili linahitaji liangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta katika mapendekezo yaliyowasilishwa hapa, Kifungu cha 34 cha Muswada kinapendekeza kuongeza Kifungu cha 78A ambacho kinaipa Bodi ya Stakabadhi Ghalani mamlaka ya kutoza faini kwa mtu anayetenda kosa chini ya sheria hii. Mamlaka ya kutoza faini sasa yanapelekwa kwenye Bodi, Wakala, ambayo yanaleta kero kubwa kwa Wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linalotaka kufanywa halina tofauti na mamlaka ambayo wamepewa *EWURA* wanatoza faini ya shilingi milioni tano na zaidi, *SUMATRA* anakutoza faini mara mbili ya tozo halali na Bodi inapewa mamlaka hayo hayo. Hiki ni kinyume kabisa na utaratibu wa utawala wa sheria ambapo Mahakama ndiyo chombo pekee kinachoweza kutoa haki na kufanya maamuzi. Tunapotoa mamlaka kwa Taasisi, Bodi au Wakala kutoza faini bila kwenda mahakamani, ni kutoutendea haki Mhimili huu wa Mahakama ambao ndiyo wenye wajibu wa kutoza faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashindwa kuelewa hapa mnapoanzisha Bodi ya Stakabadhi Ghalani, wakati huo huo Serikali ina Wakala au Bodi ya Nafaka Mchanganyiko! Toka tumepitisha Sheria ya kuwa na Bodi ya Nafaka Mchanganyiko, tumeshindwa kuwekeza mtaji kwenye Bodi hii ili iweze kununua mazao. Sasa tatizo kubwa ni soko, matokeo yake wakulima wanakopwa na hawalipwi. Hata hili mnalolifanya sasa bado litaongeza matatizo na kero kwa wakulima. Wakulima wengi wamekuwa wakipinga juu ya utunzaji wa mazao katika maghala

ambapo utunzaji wake unakuwa na tozo kubwa na hatimaye hawapati faida kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi, pamoja na maneno mazuri yanayoelezwa katika Muswada huu kwamba utawawezesha wakulima kuweza kupata mikopo kwenye Taasisi za Fedha, ningependa kujua ni wakulima wangapi ambao wamenufaika; kwa sababu mpango huu umeanza toka mwaka 2006 lakini wakulima hawapati mikopo wakipeleka stakabadhi zao ambazo wamehifadhi mazao katika ghala. Bado tunadhani mfumo huu utamsaidia mkulima. Mfumo huu hautaweza kumsaidia mkulima. Tatizo kubwa ni kwamba, ni lazima tutengeneze mpango madhubuti ama wa kuwa na wanunuzi wa mazao wanaofahamika na kuifanya biashara hii kuwa huria au Serikali ambayo inatoa bei elekezi ijipange vizuri kununua mazao ya Wakulima.

Serikali haiwezi. Tujifunze kwenye historia; tulikuwa na *GAPEX* na *NMC,* tulishindwa kufanya biashara ya mazao. Sasa ni vizuri mkaiacha biashara hii ikawa huria kuliko kuifunga wakati Serikali haiwezi. Imekopa mahindi kwa wakulima kule Rukwa, Katavi, Ruvuma, Iringa na mahali pengi na wameshindwa kulipa hizo fedha na mpaka leo Wakulima hawajalipwa fedha zao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni lazima tutengeneze mpango madhubuti ulio wazi ambao utamnufaisha huyu mkulima maskini. Huyu mkulima ni maskini, ana shida ya fedha, anatumia nguvu yake kuzalisha lakini hajui atauza wapi. Serikali inatangaza bei elekezi, lakini haina uwezo wa kununua kwa bei hiyo elekezi, inawakopa na kwenda kuweka kwenye maghala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni nani sasa atajenga hayo maghala; ni Bodi au ni Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika? Maghala yenyewe hayapo, lakini leo tunaanza kuandaa mpango wa kuhifadhi mazao katika maghala, wakati maghala yenyewe hayajajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vitu ambavyo Muswada huu hauna manufaa ya moja kwa moja kwa mkulima maskini katika nchi hii. Lazima tuangalie ni namna gani sasa tunaweza kumsaidia mkulima maskini katika nchi hii aweze kupata soko la uhakika. Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko imeshindwa kutimiza wajibu wake wa kuwatafutia masoko ya uhakika wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusudio la kutoza tozo kwa ajili ya kuhifadhi; kama mazao yatakaa ghalani kwa muda mrefu hata thamani ambayo mkulima angeweza kupata inaweza kuishia kwenye tozo la kuhifadhi. Nani anachukua dhamana ya kuangalia ubora na uhifadhi wa mazao hayo?

Gharama zinazotumika kwa kuweka dawa za kuhifadhi mazao hayo, hamjaweka bayana ni nani anabeba mzigo huu?

Kuanzisha Bodi hii na Uwakala huu wa kuweka stakabadhi ghalani, ni mpango wa kuendelea kuwakandamiza wakulima wa nchi hii na wala si kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali ilitafakari hili, wasije na majibu mepesi katika maswali magumu. Tatizo la wakulima katika nchi yetu ni kubwa mno na wala hakuna mkakati wowote ambao unaonekana unalenga kumwondoa mkulima maskini mahali alipo. Mkulima huyu hasaidiwi katika uzalishaji kwa maana ya pembejeo. Pembejeo zinauzwa bei ghali, gharama za uzalishaji ni kubwa, lakini bei ya mazao ni ndogo. Lazima kuwepo na uwiano ili tuweze kumsaidia mkulima huyu maskini katika nchi yetu. Katika miaka yote 53 ya Uhuru wa

nchi hii, wakulima wadogo wadogo hawa ndiyo wameendelea kuzalisha mazao ambayo yanalilisha Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimalizie kwa kuitaka Serikali; umefika wakati sasa wa kuwalipa wakulima fedha zao. Muda ni mrefu toka mmechukua mazao yao na mazao mengine yapo kwa wakulima bado mmeshindwa kuyanunua. Sasa hawa ambao mmewakopa walipeni! Kule Songea hamjawalipa, kule Rukwa hamjawalipa, hebu walipeni kwanza ili tuweze kuona manufaa ya stakabadhi ghalani. Kama kutakuwa na maghala na mnahifadhi mahindi lakini hamuwalipi wakulima fedha zao, hamjawasaidia watu hawa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili tatizo kwanza la madai ya wakulima ni lazima lipewe kipaumbele. Mimi ninasema kwamba, Muswada huu hauna masilahi mapana kwa wakulima maskini wa nchi hii. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtutura na ajiandae Mheshimiwa Barwany!

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa na wenzangu waliotangulia kwamba, dhamira ya Muswada huu wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani ni kumkomboa mkulima. Takribani sasa huu ni mwaka wa sita toka tupitishe Sheria hii na kuanza kutumika nchini, lakini Serikali haijafika na kutuambia ni manufaa kiasi gani wakulima wameyapata. Sana sana kila kona kuna kilio. Wamekuwa wakitoa mfano Wilaya ya Tandahimba na Newala kwamba, wamenufaika sana na mfumo huu, lakini ukienda huko bado wakulima wana kilio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitataja tozo chache tu ambazo mkulima anapambana nazo kutokana na mfumo huu. Tozo hizi asingeweza kukutana nazo kama mfumo huu wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani usingekuwepo. Kutokana na mfumo huu, mkulima anawajibika kugharamia ghala ambalo korosho zake zinahifadhiwa.

Vilevile anagharamia tozo kwa Chama cha Msingi, ana tozo ya kuchangia Chama Kikuu, Mfuko wa Maendeleo ya Korosho, ulinzi wa ghala, analipia magunia na usafiri, tozo ya Halmashauri, ulinzi wa kusafirisha fedha, unyaufu na vilevile analipia riba ya benki kwa fedha zinazokopwa na Chama Kikuu cha Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya kumsaidia mkulima hapa inaondoka. Halafu mfumo huu unazungumzia korosho zikusanywe ziwekwe kwenye ghala aje mnunuzi anunue mkulima alipwe fedha zake zote.

Kutokana na Vyama vya Msingi, Chama Kikuu pamoja na Serikali kushindwa kumshawishi mkulima aingie kwenye mfumo huu kama sheria inavyosema, matokeo yake wanakwenda kwenye mabenki, vinavyokopa ni Vyama vya Msingi vikishirikiana na Chama Kikuu, lakini riba analipa mkulima ambaye hakushiriki hata mara moja katika majadiliano kwenye kukopa fedha zile. Sasa ni kwa nini mkulima alipishwe riba kubwa ilihali yeye hakushiriki hata mara moja katika kukopa zile fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ingefuatwa kama ilivyo, kwa kiasi kikubwa ingekuwa mkombozi kwa mkulima, lakini haifuatwi. Kwa hiyo, ubovu siyo sheria, ubovu hapa ni usimamizi na utendaji wa watendaji wetu. Tumeshuhudia baadhi ya Viongozi wa Ushirika ambao walikuwa malofa tu, leo ni matajiri wa kutupwa, wakati mkulima anabaki kuwa mnyonge. Hili haliwezi kukubalika hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iende ikafanye *survey* kwa wakulima ili waone kama kweli mfumo huu wa ununuzi wa mazao unawasaidia lakini tunaendelea kuongeza sheria tu na adhabu, haisadii. Tunayo adhabu ya kifo hapa kwa mtu anayeua imemaliza tatizo la watu kuuana? Leo unasema mtu apewe adhabu shilingi milioni tano au kifungo cha miaka sita au saba, haisaidii hata kidogo na dhamira ya kumkomboa mkulima bado sijaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa hapa mwaka juzi kwamba italetwa sheria itakayoweza kusaidia endapo bei ya mazao ya mkulima itakuwa imeanguka, hiyo sheria mpaka leo haijaletwa. Mimi naamini kabisa sheria ile ingekuwa ndiyo mkombozi kwa mkulima kuliko hizi sheria ambazo tunaendelea kuleta siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzijuzi tumefanya uchaguzi, mimi nawapongeza sana wananchi wa Tunduru. Kuna kiongozi mmoja wa ushirika kimsingi alikuwa lofa tu, kutokana na mfumo huu wa stakabadhi ya mazao ghalani kajilimbikizia fedha, kanunua gari kaandika ‘usiumize kichwa’. Yaani sisi tumeibiwa halafu anatuambia tusiumize kichwa kwa fedha ambazo ametuibia na kununua gari. Wananchi wa Tunduru wakasema na wewe tutakuonyesha kwamba na wewe usiumize kichwa, wamemuengua lakini ujasiri huo wa wananchi wa Tunduru hauwezekani kupatikana kila eneo. Leo wananchi wa Tandahimba wanalia kutokana na viongozi wao kuwaibia fedha wanashindwa kuwaengua kwa sababu ya uwezo wa kifedha walionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sharia hii mimi bado sijaiona kama ni mkombozi kwa mkulima. Ukombozi kwa mkulima ni ile sheria ambayo tulisema kwamba iletwe itakayoweza kusaidia anguko la bei za mazao ya mkulima. Ile sheria ndiyo ingekuwa mkombozi kwa mkulima lakini siyo kwa sheria hizi ambazo kila siku tunabadilishiwa, tatizo siyo sheria hii iliyopo, tatizo ni usimamizi na watendaji wetu hawajawa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tozo zote hizi zinakwenda kwa mkulima. Leo mnatuambia kwamba tuanzishe na Bodi, chimbuko na uendeshaji wa hiyo Bodi gharama zake zitakuwa zinatoka wapi? Ni mkulima atakayebebeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja hii hata mara moja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Salum Barwany.

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, najikita zaidi katika Stakabadhi Ghalani hususani katika eneo la zao la korosho katika Mikoa ambayo zao hili linalimwa. Kuna kilio cha muda mrefu cha wakulima ambao wanazalisha zao hili. Pia nichukue nafasi hii kuwaambia wakulima hao kwamba juhudi kubwa ambazo zimefanywa na Wabunge wenu katika kuhakikisha kwamba zao hili linaleta manufaa ndiyo maana ya kuletwa kwa sheria hii sasa hivi katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge mwenzangu ambaye ametangulia, amechambua malalamiko na masikitiko makubwa kwa wakulima wa korosho katika kipindi chote ambacho Stakabadhi Ghalani imeweza kuwa hai. Ni kwamba sheria hii kama ilivyoletwa, sisi tulitaka iletwe katika maana ya kwamba kutafuta mwarobaini wa tatizo hili ambalo mpaka sasa wakulima wa korosho wameshakatishwa tamaa kwamba haliwezi kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wengi katika mfumo wa Stakabadhi Ghalani wamekuwa siyo wadau haswa kama inavyozungumzwa, kuna vyombo ambavyo viko juu yao ambavyo ndivyo vinavyofanya maamuzi dhidi yao. Mfano mdogo ni pale wakulima wale wanapopelekewa mazao yao katika ghala wanalalamika kwamba hata wao hawahusishwi kujua kwamba korosho zao zitauzwa bei gani. Bei dira inapangwa na nani, gharama za mkulima anazijua mwenyewe mkulima ni kiasi gani kilo moja inamgharimu mpaka kufikisha katika ghala hilo lakini matokeo yake anaambiwa tu kwamba bei dira ya mwaka huu itakuwa ni bei hii. Wanaitwa wadau mbalimbali katika vikao mbalimbali vya Bodi ya Korosho lakini vikao hivyo vyote ukiangalia kwa kina kabisa wale wote wanaoshiriki katika vikao hivyo siyo wakulima halisi wa zao hilo, hiyo inapelekea kuona ni dhahiri kabisa kwamba wakulima hawa hawashirikishwi kikamilifu katika maamuzi na hatma ya bei ya mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwazi haswa haupo. Leo unapofika katika ghala unakuta wanunuzi wa makampuni mbalimbali, tenda inapofunguliwa kuna usiri mkubwa wa wakulima kutokujua kwamba ni nani ametenda bei gani. Matokeo yake inatangazwa kwamba bei dira ya safari hii, bei ambayo imefikiwa ni kiasi hiki. Ni *top down approach* kiasi kwamba mkulima anashindwa kujua gharama zake zinaweza kulipwa kwa kiasi gani, uwazi katika hili haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika suala zima la Vyama vyetu vya Ushirika, siyo kwamba tunazuia Serikali isisimamie lakini vimepokwa kwa kiasi kikubwa usimamizi katika suala zima la mazao haya. Siyo Vyama vya Wakulima haswa kama inavyofikiriwa ni Vyama vya Viongozi wa Serikali ambao kwa kiasi kikubwa wale viongozi wao wanatumika tu kuhakikisha kwamba wanapata maslahi. Leo ukiangalia kwa kiasi kikubwa walionufaika na Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni viongozi wetu wa Serikali. Unaona kwamba kuna huruma unastaajabu, leo Serikali hii inasema kwamba wakulima wamepata bei bora mazao yao, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani unawasaidia hauwezi kuachwa huu, ndiyo mwarobaini wa wakulima lakini unamwangalia nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali inakuwa na huruma zaidi na mkulima huyu ambaye tayari maandalizi ya shamba lake mpaka kufikia hatua ya kupata zao hilo Serikali iko pembeni lakini inapofika katika msimu wa mauzo, Serikali tayari imeshapeleka mikono yake, imepeleka kifua chake na kuona kwamba inawahurumia wakulima hawa kitu ambacho siyo kweli kwamba mkulima hapa anatakiwa pale tu anapopeleka mazao yake katika ghala lakini pale anapoandaa Serikali haipo. Leo utamkuta mkulima mpaka dakika ya mwisho pembejeo hazijui ziko wapi, utaratibu uko namna gani wa zao hilo lakini mwisho wa siku tayari anapangiwa taratibu za namna ya kuuza korosho zake. Hizo ni huruma tu ambazo tayari wale wanaohurumiwa wanajua kuwa hii ni danganya toto tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu hapa Mbunge wa Tunduru amezungumzia suala la gharama na makato mengi kama tozo ambayo hayamshirikishi mkulima. Pesa ambazo zinachukuliwa benki hajashirikishwa, ununuzi wa magunia hawajashirikishwa na kadhalika. Sisi tunafahamu wale ambao wanafanya biashara za mazao, anapokwenda kununua mazao kwa mkulima anakwenda na sehemu ya kuhifadhia mazao yake, anakwenda na magunia, anakwenda na kila kitu ambacho kitamfanya mazao yake yawe salama lakini mkulima wa korosho na wakulima wengine wanatakiwa wao wanunue sehemu ya kuhifadhi mazao yake, mwenye haja ni yule ambaye tayari anaona ni namna gani bidhaa yake aliyonunua kwa mkulima ataihifadhi. Hivyo gharama nyingi ambazo zinatozwa kama tozo kwa mkulima siyo za lazima kwa mkulima na matokeo yake hata hiyo bei ambayo inapangwa karibu 30% inakwenda katika gharama ambazo mkulima huyu hazimhusu hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema kwamba bado Mfumo wa Stakabadhi Ghalani unaendeleza utaratibu wa kuuza korosho ghafi, bado haujaleta taratibu maalum ambazo

zinaweza kumkomboa mkulima na kuleta ajira katika nchi yetu. Tuna viwanda kadhaa zaidi ya 12 lakini ukienda *BRELA* utaona ni kina nani wamiliki wa viwanda vile, ni Viongozi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ni viongozi wa Serikali Kuu ndiyo waliobinafsishiwa viwanda vile. Hapa amezungumziwa Mheshimiwa Kigoda, yeye ndiye alikuwa ni mratibu mkubwa wa ubinafsishaji wa viwanda vile, anajua viwanda vile vinamilikiwa na nani? Ndiyo maana mpaka leo utaratibu rasmi wa viwanda vile kuweza kufanya kazi, vikazalisha na wananchi wakapata ajira ya kutosha, Serikali inafumbia macho tukiamini kabisa kwamba utaratibu wa kuuza korosho ghafi katika nchi ya India ni mafanikio kwa viongozi wetu ambao tayari wana 10% katika mfumo mzima. Hii ndiyo inapelekea utaratibu wa kuweza kufanya hivi vikafanya kazi, vikaleta ajira kwa wananchi wetu hususani kina mama ambao ndiyo wafanyakazi wakubwa katika viwanda vile, Serikali inafumbia macho na kuendeleza mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani ambao hauleti matumaini makubwa ya viwanda vile kuweza kufanya kazi. Hili ni tatizo kubwa, tulitarajia sasa sheria hii ingekuja na mwarobaini kamili wa kuwapa matumaini wakulima ili waone kwamba Serikali yao inajali maslahi yao lakini kwa matatizo haya ambayo bado yanaendelea kuwepo na naamini kabisa kwamba matatizo haya yataendelea kuwepo siku nenda rudi kama bado Serikali haijakaa na wakulima wenyewe kuhakikisha kwamba wanapata fedha bora katika mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho nizungumze katika suala zima la namna gani wakulima wetu wadogowadogo hawa, mkulima mkubwa atakuwa na gunia 30, 40 mpaka 50 lakini kwa idadi kubwa wakulima wetu wanakuwa na kilo 30, 40, 50 unapomweka huyu alipwe baada ya miezi unatarajia nini? Mahitaji yake yako karibu pale, anataka kupeleka watoto shule, anataka aandae shamba lake, anataka kuandaa nyumba yake hivyo mpaka atakapokamilisha malipo ya majaliwa hayo inamchukua miezi sita mpaka bajeti yake inavurugika haielewi mwisho wa msimu anajiuliza pesa hizi nimezifanyia nini kwa sababu mapato yake hayakidhi haja ya bajeti ambayo anakuwa nayo. Hivyo, kitendo cha kuwalipa wakulima kiasi kidogo kidogo kwa zaidi ya awamu tatu hakimpi tija. Tungeitaka Serikali na Serikali inaweza, tunasikia leo Serikali inanunua mahindi huko mamilioni kwa mamilioni, kwa nini Serikali isijipige kifua ikatoa kiasi kikubwa cha fedha, ikanunua korosho kwa wakulima halafu baadaye korosho hizo zikasubiri bei ili wananchi hao wakapata moyo wa kuweza kuendeleza zao hili. Zao hili katika nchi yetu linatupatia fedha za kigeni kwa kiasi kikubwa ambazo ndizo tunanunua dawa, tunanunua mashangingi ya viongozi wa Serikali, tunalipwa posho kutokana na pesa za wakulima wa korosho lakini mkulima wa korosho hathaminiwi kama tayari ana mchango mkubwa ndani ya Taifa lake. Hivyo tungeitaka Serikali sasa itengeneze Mfuko Maalum kwa sababu Mfuko huo utawezesha sasa wananchi kujinasua mapema katika bei na pesa zao zikaanza kufanya kazi zile ambazo tayari wao wana matarajio nazo kwa ajili ya maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nasema siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii muhimu ambayo inagusa sana malalamiko ya muda mrefu ya wakulima Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la Serikali hii kila siku kuleta sheria mbalimbali ambazo zinahusiana na wakulima lakini hawatatui tatizo la msingi la wakulima. Tatizo la msingi la wakulima siyo idadi ya sheria hizi ambazo zinaletwa. Kwanza, usimamizi wa sheria katika nchi hii uko chini sana lakini pili, unapozungumzia malalamiko ya Watanzania wakulima na wazalishaji kwenye mfumo mzima wa Stakabadhi Ghalani kwa kiasi kikubwa siyo sheria. Tatizo kubwa ni usimamizi wa mfumo wenyewe kwamba, kuna mambo ambayo kwenye sheria hayamo lakini ndiyo yanafanyika. Kwa mfano, wenzangu wamezungumza, viongozi kule chini kwenye Vyama

vya Msingi wakishirikiana na Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa na Bodi zenyewe hizi pamoja na baadhi ya viongozi Serikalini wanatengeneza genge ambalo linamlazimisha mkulima kwamba ili aweke mazao yake ghalani ni lazima apitie kwenye Chama cha Msingi, Chama ambacho kwa kiasi kikubwa kinamgharimu mkulima bila sababu. Mifumo ya Stakabadhi Ghalani kwenye nchi nyingi duniani ni kwamba ghala liko pale, mkulima au kikundi cha wakulima ambao wamekubaliana wenyewe wanaweza kupeleka mazao yao kwenye ghala kama mmoja au kama kikundi. Siyo lazima kumshinikiza hata mtu ambaye siyo mwanachama wa chama chako apitie chama chako, haiwezekani! Kwa hiyo, kuna tatizo la uzembe mkubwa wa Wizara kusimamia mambo haya kwa sababu huu ni uvunjifu wa sheria na Waziri, Naibu Waziri na Bodi zenyewe zinafahamu kwamba sheria hailazimishi hicho kitu, hilo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, nimeona nirudie kulizungumza kwa msisitizo, njia pekee itakayoweza kututoa kwenye malalamiko ya soko kwa wakulima ni kuanzisha *Commodity Exchange Market,* kuanzisha soko la mazao. Duniani kote kwenye nchi ambazo wamefanikisha mipango ya masoko wana kitu hicho, sasa Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda, kila siku wanapiga chenga wakulima wanakosa mazao. Ukitengeneza mfumo wa *Commodity Exchange Market* maana yake una-*operate* kama *stock market*, una *operate* katika namna ambayo bidhaa ambazo ziko kwenye ghala duniani kote uwe Dubai, Ufaransa au wapi unaweza uka-*access* kiasi kwamba ukiangalia *trend* ya ghala, unaweza hata ukatabiri kwamba mwaka kesho kwa *trend* ya ghala hili katika mazao haya naweza kununua zao fulani kwa kiasi fulani. Sheria hiyo tangu mwaka 2006, Serikali hii walianza utaratibu wa kuianzisha ni bahati mbaya sana kwamba kuna baadhi ya wafanyabiashara katika nchi hii ambao wanatengeneza fedha nyingi kutokana na upungufu huu wa kisheria wakasababisha Serikali ipigwe ganzi kutengeneza sheria hiyo. Kwa hiyo, mpaka leo tangu 2006 miaka takribani 10 bado Serikali inavuta miguu kutengeneza sheria itakayosababisha wakulima wazalishaji wapate bei stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Sheria ya Mabadiliko ya Sheria ni kama wameandika Sheria upaya kabisa, haya siyo majibu ya kero za wakulima ambao wanatumia stakabadhi ghalani. Majibu ni kwamba wakulima hawa wanataka ushindani wa wanunuzi na ushindani wa wanunuzi unaweza kuwa *guaranteed* kwenye mfumo ambao ni *Commodity Exchange Market,* nje ya mfumo huo mtabaki kila siku Serikali, Wizara ina-*gang* na Bodi hizi, wanashirikiana na baadhi ya wafanyabiashara ambao kila siku wanatumika kwenye kupanga bei na kuhakikisha kwamba mkulima anauza mazao yake kwa bei ambayo imepangwa kwa njama za Bodi na Serikali yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uchumi wa soko huria, leteni Sheria ya *Commodity Exchange Market* ili kusudi pawepo na uhuru, watu washindane kwenye kununua. Leo watu ambao wananunua korosho na mazao mengine kwa kiasi kikubwa ni walewale. Ni walewale kwa sababu utaratibu mzima wa kupanga bei elekezi, utaratibu mzima wa kutoa leseni za ununuzi unaamuliwa na Bodi, unaamuliwa na vyombo ambavyo kimsingi madhumuni yake katika uendeshaji hayana tija kwa mkulima. Ilipaswa kila anayetaka kununua akanunue, kuna sababu gani ya kutoa leseni kwa mnunuzi? Kwa nini msiache kila anayetaka kununua akanunue? Bidhaa iko kwenye ghala anayetaka kununua akanunue, hakuna ulazima wa kuweka mfumo wa kirasimu wa kuamua wanunuzi, zote hizi ni njama za rushwa. Ndiyo maana wenzangu wanalalamika kwamba watu ambao wako kwenye mtandao huu kuanzia kwenye Bodi na Vyama hivi wanatajirika kuliko wakulima, wakulima wananyong'onyea wao wanatajirika, haiwezekani! Hii Serikali sijui inataka tuseme kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kumsihi Mheshimiwa Dkt. Kigoda, nilizungumza hata kwenye Kamati na narudia kuzungumza tena. Hii sheria haitatui kero yoyote ile katika matatizo ya wakulima, cha kufanya ni usimamizi na udhibiti wa kero ambazo

wakulima wanazo ambazo kimsingi kwenye sheria hazipo kwa kiasi kikubwa. Tunataka Kanuni za utekelezaji ili kuboresha usimamizi zitengenezwe katika kiwango cha kutosha lakini la pili zikamilike kwa muda muafaka. Serikali hii kuna tatizo la kuandaa Kanuni pale sheria inapokuja kwa maslahi ya wananchi wengi na inakuwa dhidi ya wafanyabiashara wenye pesa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mifano na hii ni dharau kwa Bunge. Katika vikao vya mwaka 2010 ilipitishwa sheria hapa ya kutaka migodi yote ya madini iorodheshwe kwenye Soko la Mitaji kwa lengo moja au mawili. La kwanza ili kusudi mapato yao yawe wazi, tunaibiwa miaka yote kwa sababu mapato ya migodi hayako wazi. Hiyo sheria ilitungwa wakati wa Mheshimiwa Ngeleja na mpaka ameondoka ameshindwa kuandika Kanuni. Amekuja Mheshimiwa Profesa Muhongo, Mzee wa Viwango mpaka anaondoka hajaandika kanuni. Leo amekuja Mheshimiwa Simbachawene na ana miezi michache ataondoka, miaka mitano sheria ya Bunge haiandikiwi kanuni, hii ni aibu, hii ni Serikali gani? Sheria Bunge limepitisha kanuni hamleti na siyo hiyo tu, kuna Sheria ya Mawasiliano, hakuna watu wanaotengeneza pesa nyingi katika nchi hii kama kampuni za simu, wanatengeneza mabilioni ya shilingi lakini Serikali hii haina uwezo wa kujua kwamba ni kiasi gani ambacho makampuni haya yamepata ili kusudi ipate kodi sahihi. Mnabaki kuwa Serikali ya kimaskini wakati mna vyanzo vingi, hamtekelezi kwa sababu ya rushwa tu, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya kutengeneza sheria hiyo ya *Postal and Telecom Act,* 2010 mpaka leo miaka mitano hazijaletwa wanataka nini hawa? Ni wizi mtupu, *ESCROW* kila eneo, haiwezekani! Tunataka kanuni zifike mahala tuwe tuna muda maalum kwamba katika kipindi hiki, Wizara sheria yake ikipitishwa kanuni ziletwe, tofauti na hapo hili Bunge linapoteza maana ya kuwepo kwa sababu mamlaka ya Kikatiba ya kutunga sheria ni ya sisi kama Bunge lakini mamlaka ya kutengeneza kanuni ni ya Mawaziri kama Serikali. Tunatengeneza sheria, kanuni haziletwi, sasa kama kanuni haziletwi tafsiri yake ni kwamba sisi kama Bunge ambao tumetunga sheria hiyo tuna maana gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi napenda kuwaambia kwamba wakulima wa Tanzania wana masuala ya msingi ambayo yanatakiwa yafanyiwe kazi…

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWEYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila hebu subiri kidogo. Mheshimiwa Kitwanga.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimpe taarifa Mheshimiwa anayezungumza kwamba *Geita Gold Mine* iliji-*list* katika Dar es Salaam *Stock Exchange* lakini kutokana na wananchi kutokuwa na mitaji mizito zilizopatikana ni dola elfu arobaini tu. Kwa hiyo, makampuni haya yako tayari ku-*list* lakini watu hawako tayari kwenda kununua *shares*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila!

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe elimu tu kwamba sheria ilisema mtengeneze kanuni za kutaka migodi i-*list* kwenye (*Dar es Salaam Stock Exchange - DSE*). Nilitegemea majibu ya Serikali iwe ni kwamba tumekwishakuandika kanuni, miaka mitano hamjaandika kanuni, mnakuja na majibu ya ujanja ujanja. Bunge linataka kanuni za migodi ku-*list share* zake kwenye *stock market* hasa *DSE* ziletwe, kwa nini hamtaki kuleta? Hamjaleta kanuni! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna majibu ambayo yanatolewa kwa ujanjaujanja kwamba sijui mgodi gani ume-*list*! Kuna tofauti kati ya *cross listing* na *listing*. Kuna baadhi ya migodi wame-*cross list,* hizi ni tofauti Mheshimiwa Waziri unapaswa kuzijua hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Tanzania moja ya matatizo yao makubwa ni kuingizwa kwa mazao kutoka nje kinyemela. Kuna utaratibu unasema kwamba tukiwa na *shortage* ya chakula watu waagize chakula kutoka nje lakini vibali vya kuingiza chakula kutoka nje vinatolewa kinyemela, matokeo yake unakuta kuna ma-*godown* yamejaa mchele kutoka nje wanashindwa kushindana na wazalishaji wa ndani. Matokeo yake wakulima ambao Serikali imetoa matrekta na kuwasaidia hapa na pale, wanakosa tija ya mazao yao kwa sababu bandari ya Dar es Salaam inaachwa uchi, bandari bubu zipo kibao. Nimetoa mfano hapa kutoka Bagamoyo mpaka bandari ya Dar es Salaam ni kilomita sabini tu, kuna bandari bubu 32, watu wanaingiza mizigo bila utaratibu. Mazao haya yanaingia ndani, yanashindana na mkulima ambaye amezalisha bila ruzuku, katika hali ya kawaida huyu mkulima huwezi kumkomboa. Serikali idhibiti mifumo, acheni kutoa vibali kinyemela, mnamuua mkulima, mnakuja mnadanganya na sheria, kanuni, taratibu, lakini haya ndiyo maeneo ya kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeua viwanda kwa mfano, wametoa mfano kwamba Mheshimiwa Kigoda ndiye alikuwa Waziri wakati wa kuuzwa viwanda hivi. Viwanda vimeuzwa kwa bei ya kutupwa. Mheshimiwa Lukuvi akiwepo hapo mwaka juzi niliwauliza ni lini mnarejesha viwanda hivi, ili kuongeza thamani ya mazao ni lazima uyachakate. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mkapa, jiandae Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami naomba nichangie kuhusu Muswada huu wa Mabadiliko ya Sheria ya Stakabadhi Ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge wa Mkoa wa Mtwara tunapoona maua ya korosho yanaanza kutoka tunapata matatizo sana tunajua sasa ndiyo matatizo ya Ubunge yanapoanza. Kwa sababu zao la korosho linapoanza kuuzwa maswali yanakuwa mengi sana ambayo hatuna majibu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa Nanyumbu na nachokisema hapa nimeagizwa na wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu. Wakulima wa zao la korosho Wilayani Nanyumbu wanakereka sana na mtindo huu wa Stakabadhi Ghalani wanaona hawanufaiki na hauwanufaiki siyo kwa sababu ya mtindo wenyewe ni kwa sababu utekelezaji wa mfumo huu ni mbovu sana. Ni mbovu kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema wenzangu hapa waliotangulia, korosho mkulima anapeleka leo hii mwezi wa tatu malipo atayapata mwezi wa saba. Wamezungumza Wabunge wenzangu hapa kwamba hii ni kero kubwa sana kwa mkulima hasa ambaye hali yake ni duni kabisa, ana mahitaji mengi lakini tayari ameshapeleka zao lake ghalani na hapati malipo yeyote ndani ya muda ambao anafikiria yeye atapata. Shida ni nyingi, afya wanauguzana huko hawana hela korosho iko ghalani! Watoto wanakwenda shule, tunapata taabu sana sisi kuombwa misaada ya ada za shule, siyo kwa sababu hawana hela ni kwa sababu pesa yake hajalipwa. Kwa hiyo, tunapata taabu sana wakati wenyewe wana rasilimali yao wanaipeleka ghalani. Vilevile mazao haya huwa yanapotea huko njiani, yanaibiwa lakini wanaopoteza hawachukuliwi hatua yeyote, bado mzigo unakuwa kwa mkulima halipwi pesa yake. Kwa hiyo, mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani kwa kweli Wilayani Nanyumbu bado haujawa mzuri na

wananchi wanalalamika sana na mimi nimekuwa nikiwajibu majibu ambayo kwa kweli hayaleti matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulipa kwa awamu ni tatizo lingine. Mheshimiwa Barwany amezungumza, Mheshimiwa Mtutura amezungumza, hivi kwa nini hatuwalipi hii pesa mara moja tukabakiwa na yale malipo ya majaliwa? Mbona sisi tunalipwa mshahara mara moja tu hatulipwi nusunusu? Kwa hiyo, huu mtindo wa Stakabadhi Ghalani wa kuwalipa wakulima nusunusu nao hauna tija kwa mkulima mwenyewe kwa sababu anashindwa kupangilia mambo yake kwa ufasaha. Mkulima hajui bei ya korosho, yeye anaambiwa tu pesa zako hizi hapa lakini kwenye mnada hausishwi, hajui korosho yake imeuzwa kwa bei gani, kwa hiyo ni mtu tu anapitwapitwa tu na mambo ambayo yeye hashirikishwi kiujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna mgongano wa kisheria, kuna Sheria ya Korosho, kuna Sheria ya Stakabadhi Ghalani na kuna Sheria ya Ushirika, sasa hili zao la korosho litasimamiwa na sheria ipi? Haya ndiyo matatizo ambayo wanayapata wakulima wa zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni kwamba maghala haya ya korosho yako mbali na wakulima. Nanyumbu mpaka Mtwara ni kilomita takribani 200 hasa kinachotokea huko njiani, mkulima amepeleka korosho yake safi lakini wataongeza uchafu mwingine huko, mwisho wa siku mkulima ndiyo anayepata adhabu. Siyo kosa lake ni kwa sababu maghala haya yapo mbali sana na zinakotoka korosho zenyewe. Kwa hiyo, udhibiti unakuwa ni mgumu, mkulima anakuwa hajui ni nani aliyepoteza na kwa nini yeye aadhibiwe kwa kosa la mtu mwingine. Nachoomba ni kwamba korosho zinapopotea njiani wakulima wafidiwe mara moja, isiwe mzigo tena kwa mkulima ndiye afidie zao hilo la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile malipo ya majaliwa yanatofautiana kutoka sehemu hadi sehemu, hii nayo ni kero kubwa sana. Hata Wilayani kwangu Namnyumbu imetokea hivyo sehemu nyingine wanapewa pesa nyingi na sehemu nyingine wanapata pesa kidogo, hii dhuluma yote inamwendea mkulima. Hivi huyu mkulima wa korosho ana kosa gani kwa zao lake la korosho, mbona mazao mengine hayana matatizo kama haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni kwamba elimu kwa ajili ya mfumo wa Stakabadhi Ghalani bado haijawafikia vizuri wakulima. Naomba Wizara ya Biashara na Viwanda, Wizara ya Kilimo zijitahidi kupeleka watu huko Mikoani kutoa elimu hii ili wakulima waweze kuelewa kwa ufasaha. Hawa wanaosimamia bei, wanaosimamia maghala ndiyo walitakiwa watoe elimu kwa wakulima lakini elimu hii haitoki na wakulima wanabaki solemba hawajui kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema Mawaziri msikae maofisini, naomba mje Mkoa wa Mtwara msikilize matatizo ya wakulima. Matatizo ni mengi sana kuhusu zao la korosho, pembejeo hazifiki kwa wakati, pembejeo zinauzwa bei ghali kiasi kwamba mkulima hawezi kuzimudu na wanaolangua wanafahamika lakini Serikali inashindwa kuwachukulia hatua! Nanyumbu hali siyo nzuri, wakulima kwa kweli mtindo huu wa Stakabadhi Ghalani hawautaki, watautaka pale tu ambapo ufanisi utaongezwa ili mkulima huyu aweze kunufaika na zao hili la korosho. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mangungu na baadaye jiandaeni Serikalini.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaweza ikafika wakati sisi wenyewe tukajiuliza na tukajishangaa. Kuna madai mengine katika uchangiaji wetu yanakuwa hayana msingi sana. Sijawahi kufahamu kama kuna utaratibu wa Waziri anayehusika kuleta kanuni za uendeshaji au zinazotumika kwa sheria fulani zije kujadiliwa Bungeni. Kama inafanyika hivyo basi ni vizuri mtuletee ili tuweze kuzipitia hizo kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu na kwa kuzingatia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba katika aya ya tatu, mazao ambayo yatahusika kwenye utaratibu huu itakuwa ni mazao yote ukijumuisha korosho, kahawa, ufuta, mahindi, mpunga na mbaazi. Sina uhakika sana, kwenye sheria hii ukienda kwenye kile kifungu cha 2 mmetoa tafsiri ya maneno mbalimbali, lakini moja ambalo nilitaka nizungumzie mmesema kwamba kuna kitu kinaitwa *shrinkage,* sisi kwa Kiswahili labda ambacho kinaweza kuwa ni sanifu zaidi tunasema unyaufu. Mmeshawahi kujiuliza ufuta unanyauka kwa kiasi cha asilimia ngapi baada ya kuwekwa? Ufuta unapoteza zaidi ya asilimia kumi hadi kumi na tano. Ina maana kama umenunua au umehifadhi ufuta kilo kumi baada ya mwezi ule ufuta umeshakuwa ni kilo tisa, mzigo huu mnampelekea mkulima. Wenzetu ambao mnahusika na usimamizi wa masoko mbona mnatupa mzigo mzito sana? Kwa maana kwamba tunaweka mifumo ya biashara huria lakini hapohapo tunaweka mfumo mwingine wa kuzuia sasa mazao haya yasifike katika soko huria. Mimi nadhani utaratibu huu ulikuwa ni mzuri sana lakini unahitaji maboresho ambayo yatamfanya mkulima asiweze kubebeshwa mzigo usiomhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho haya ambayo yameletwa hii leo, mengi sana yanazungumzia mfumo wa kurekebisha adhabu ambazo anaweza akapata yule mwendeshaji. Mfumo huu ungeweza kuwa ni mzuri sana pale ambapo mkulima amepeleka mzigo wake katika ghala, kipindi ambacho soko bado halijaweza kupata thamani ya kutosha. Mathalani, leo hii nikipeleka ufuta wangu kwenye soko kilo itakuwa ni shilingi elfu moja lakini nitakaposubiri soko litakapokuja kufikia vizuri kilo inafika shilingi elfu mbili. Kwa hiyo, napewa risiti kutoka katika ile ghala na naitumia ile risiti kama *collateral* katika benki ambayo naweza kuchukua mkopo, watani-*charge* kwa riba ya asilimia fulani ambayo tutakubaliana ili soko litakapopanda mimi nitaweza kupata pesa zaidi. Ndivyo ambavyo hata huko Ethiopia ambako pamesifiwa kwamba wameanzisha *Commodity Exchange,* mfumo unaotumika ni huo na wao *study* yao ya kwanza walikuja kuifanya hapa, wakaenda kuutumia huu mfumo wakauweka vizuri na unatumika hivi sasa lakini hapa kwetu mfumo wa masoko hauko sahihi. Bei ya bidhaa ambayo inauzwa Dodoma huwezi ukalinganisha na bei ya bidhaa ambayo inauzwa Singida, inatofautiana sana. Sasa tunaweka mfumo huu lakini hatuelewi kwamba kwa kiasi kikubwa tunamkandamiza mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu vipengele vingi vimeelezewa lakini hivi mkulima anawajibikaje na gharama za uhifadhi? Mkulima anawajibikaje na gharama za *handling*? Mkulima anawajibikaje na gharama za ukopaji wa pesa benki ambapo mnunuzi ameenda kuchukua dhamana benki kukopa pesa ili aje kununua mazao, anapewaje mkulima? Ni jambo la kustajaabisha sana bei hata ya kiroba au gunia unaweza ukakuta kwenye soko ni shilingi mia tano, mkulima anachajiwa gharama ya gunia shilingi elfu tatu, hili ni jambo ambalo halikubaliki! Naishauri Serikali kwamba waangalie vizuri mfumo huu, uwekwe utaratibu ambao mkulima atanufaika na mazao yake hasa kwa kuzingatia Serikali haitoi *incentives* zozote kwa wakulima katika kilimo. Hawana ruzuku ya pembejeo, hawana ruzuku nyingine yoyote ambayo unawalazimisha sasa waingie katika mfumo kama vile hawa watu wamepata msaada kutoka mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tumelizungumzia hapa katika Muswada huu ambao umewasilishwa, imeelekezwa ni namna gani ambavyo mwendeshaji wa maghala haya anaweza kupata leseni. Mimi naomba tuongezee, pamoja na kuthibitisha kwamba

mwendeshaji wa ghala hilo amekodi eneo na linafaa kwa uhifadhi, pia kiongezeke kipengele ni lazima kila mwendeshaji aweke bima. Unatokea wizi, unaweza ukatokea moto au maafa mengine yoyote ambayo yanaweza kupelekea hasara kwa mkulima, haiwezekani ukaweka mfumo huu watu wakapeleka mali zao bila kuwekea bima. Kwa hiyo, ni lazima iwekewe bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, pamoja na uzuri wa mfumo huu ambao umeletwa hapa na sheria hii, mimi nimeipitia vizuri sana hii sheria ambayo imepitishwa mwaka 2005 na kusainiwa na Rais mwaka 2006 na *amendment* ambazo wamezileta, sijaona upungufu mkubwa ambao unaweza kutia shaka. Wasiwasi wangu mimi ni kwamba wananchi wawe huru kufanya biashara wanayoitaka. Nimelima ufuta wangu, nimelima korosho zangu, nimelima mbaazi zangu, niamue ni wapi naenda kuuza, iwe nitauza kwa hasara au kwa faida. Aidha, mfumo huu pia uainishe pamoja na uhuru ambao utakuwa umetolewa basi wafanyabiashara wale wasitumie nafasi hiyo kuwakandamiza wakulima. Ni lazima mfumo huu, maghala haya yatumike kuwasaidia wakulima kufanya bishara zao inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja hii kwa kuwa marekebisho yaliyoletwa yalikuwa ni muhimu lakini tutoe uhuru kwa wakulima waweze kuamua wapi wanataka kupeleka mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Bado Waheshimiwa wanaleta maombi, lakini muda wetu ni mdogo sana na bado kuna upande wa Serikali na wana majibu mengi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Susan dakika tano na Mheshimiwa Musa dakika tano.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia hizo dakika tano. Napenda kuchangia Muswada huu, yaani kwanza Muswada huu wakati unaletwa hapa na marekebisho hayo bado hali ni ngumu sana kwa wakulima wa Tanzania, hususan Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Morogoro ni Mkoa ambao kwa Taifa hili unasema ni ghala la chakula, lakini mpaka leo bado Sheria zilizopo hazijawasaidia wakulima katika Wilaya mbalimbali, hususan nikizingatia mazao ya kilimo kama mpunga. Vile vile sijui Muswada huu unawasaidia vipi wakulima wa miwa, wao hawana Stakabadhi Ghalani, lakini bado wana shida kubwa katika kupandisha viwango vya mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Muswada huu umeletwa na Waziri mwenye dhamana ambaye anahusika na viwanda, Muswada huu unahusiana vipi na uboreshaji, uimarishaji wa mazao katika kupandisha thamani kwa kuweka viwanda ambavyo mazao hayo yatapata thamani kwa mkulima katika maeneo yanayotoka mazao hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukulia mfano, Ifakara, Kilombero, Wilaya ya Kilombero wamesema kwamba, wanaanzisha Stakabadhi Ghalani kuhusu mazao ya Mpunga, lakini hali halisi ikoje; watu walijitahidi, wakaunda ushirika, wakaweka mpunga kwenye maghala, matokeo yake! Bora wangeuza moja kwa moja wakati ule wanavuna kuliko wakati wanasubiri kuuzwa, mazao yako ghalani na ushirika, Serikali ikaleta mchele kutoka nje wakaulundika sokoni! Matokeo yake mpunga haukuuzika tena!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushahidi! Benki ya *NMB* walijitahidi kuwakopesha wakulima kwa kujua kwamba, Serikali itapandisha thamani ya mazao. Matokeo yake watu walikopa,

wakaenda kulima, mazao wakapata mengi na pale *KPL* wakapata mazao mengi, mpunga ukalundikana, bei ikaporomoka kwa Serikali kuleta mchele kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashangaa hii Sheria itatusaidia nini katika matatizo hayo? Je, hapo tatizo lilikuwa Sheria au mfumo mbovu au usimamizi mbovu wa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na kuwa, mtaweka Sheria nzuri kwenye maandishi, lakini kama utendaji unakuwa mbovu haimsaidii mkulima. Sasa ni bora kuboresha utendaji kuliko kutuletea Sheria kila kukicha wakati Sheria zilizopo haziheshimiwi! Watendaji wanafanya mambo ya kutisha! Leo hizo njia za panya, kwa mfano sukari, wanaleta sukari, ukiuliza vibali, wana-*photocopy* vile vibali! Kwa nini mnatoa vibali? Mmefanya utafiti wa kutosha kiasi gani, mpaka mkakuta mazao hapa nchini hayatoshelezi kwa chakula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Sheria hii itakuwa nzuri kama mfumo wa utendaji mtauboresha. Kuanzisha Bodi, hizi Bodi hazilimi! Bodi zinategemea wakulima wakiweka mazao ghalani na wenyewe wapate hela kule, zile tozo. Matokeo yake wanalipana posho, wanalipana mishahara, lakini mkulima kule anazidi kudidimia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba chonde chonde Serikali, hebu mngeonesha mfano mzuri kwa wakulima hawa ambao kila kukicha wanazidi kuwa maskini kwa sababu, mazao yao hayaongezwi thamani. Nachukua mfano, Wilaya ya Kilombero wanalima Kata zote 35 mpunga, lakini hakuna umeme, kwa hiyo, mkulima hana uwezo wa kuuza mchele, anauza mpunga ambao una gharama ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakulima kule wamejianzishia mpango wao, hawana mpango wa Stakabadhi Ghalani! Anatoa mazao yake shambani anakwenda kupiga *stock* kwenye mashine. Kwa hiyo, mnunuzi akija anakwenda kupatana naye bei pale, kwa hiyo, hana gharama; gharama ya yule mkulima ni kukoboresha mpunga kwenye mashine, kwa hiyo, halipi hela ya mlinzi! Unaona mfumo ulivyokuwa mzuri huu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi mnaleta Stakabadhi Ghalani, halafu mum-*charge* sijui hela ya ulinzi, mumchaji na vitu vingine, mwenye mashine hana mpango huo! Kwa hiyo, mkulima anasikilizia bei imepanda kiasi gani? Anakwenda kwenye mashine alikopiga-*stock* ya kukoboa mpunga anakwenda anauza, anapata hela zake! Sasa hii Stakabadhi Ghalani! Halafu mnawachangisha watu wajenge maghala huko Kijijini! Ushirika!

Ndugu zangu, mkulima ana mateso makubwa ndani ya nchi hii; naomba muweke mtandao mzuri wa kuwasimamia wakulima wakopesheke kwenye mabenki. Leo mkulima hakopesheki tena kwenye mabenki kwa sababu, bei ya mazao haisaidii, basi, wekeni! Ninyi muanzishe Mfuko, tuliwaambia hapa anzisheni Mfuko wa kulinda mazao ya mkulima bei inapoporomoka, Serikali iwe na Mfuko Maalum ili mkulima huyu asipate hasara, lakini kama hamna Mfuko huo, bei itazidi kuporomoka, leo kilo ya mchele kule Mngeta inauzwa mpaka 400/= kweli jamani kweli! Kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kibaya zaidi huu mchele mnaoagiza kutoka nje, unaletwa na huo wa sehemu nzuri unachanganywa, unauzwa bei ya juu. Matokeo yake mchele wetu unakuwa hauna soko! Wanasema mchele mbaya, kumbe umechanganywa na mchele kutoka nje ambao hauna viwango!

Mheshimiwa Mwenyekiti, rekebisheni, wekeni mkazo katika kusimamia, wekeni mkazo katika utendaji. Sheria peke yake hazitasaidia chochote bila utendaji kuimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni huu. Ni kilio kikubwa kwa Watanzania kwa kweli, tunateseka. *(Makofi)*

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hizi dakika tano na *Inshallah*, nitazitumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niunge mkono marekebisho haya tuliyoletewa ya stakabadhi ghalani yakiwa na maana ya kwamba, yanaweza yakasaidia mfumo tuliokuwa nao. Naunga mkono, ila tu nahisi *impact* yake inaweza isionekane! Yaani faida inaweza isionekane, lakini iko *excellent,* isipokuwa tuna tatizo na tatizo tulilonalo ni sawasawa na mtu kutengeneza *dining* nzuri halafu akasahau kutengeneza *washroom,* ndiyo tatizo tulilonalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tunatakiwa lazima kama tunataka kuwakomboa wakulima, maana sizungumzii korosho kwa sababu korosho ni *part* ndogo, lakini ukitazama kwamba, kuna mazao mengi sasa hivi kwa huku tunakoelekea na jinsi watu wanavyohamasisha wakulima, basi tulikuwa tunatakiwa lazima tuwe tuna-*commodity exchange;* hiki ndicho kitu ambacho kinaweza kikatusaidia kuondosha haya matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukawaambia watu walime, wakalima vizuri, ukachukua mazao yao ukayaweka ghalani, halafu kuna *charge* zitakuwa zinakuja za kuyahifadhi yale mazao pale ghalani, ukazirejesha kule kwao na huku ukiwa unaendelea kutafuta soko wakati kumbe ulikuwa una nafasi nzuri ya kuwa na masoko au minada ya Kimataifa ambayo itakuwa inatambulika ulimwengu mzima. Wewe hili ukaliacha ikawa sasa unahangaika, hatutafika!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mfano mzuri wa Ethiopia, wao walianza kinyumenyume, lakini walikuwa sahihi. Walianza na kutafuta hii minada ya Kimataifa, yaani *commodity exchange,* masoko haya, baadaye ndiyo wakaona sasa kumbe *demand* imekuwa kubwa, sasa tutengeneze hizi stakabadhi za kwenye ghala, ili kuwarahisishia wakulima mazao yapo wayalete pale. Lengo lilikuwa ni kuyakusanya ili waweze kuwa na soko la uhakika kwa hao watu ambao wanawanadia hayo mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunataka tuweze kuwa na mwelekeo mzuri na watu waweze kulima vizuri, ni lazima tuwe na minada ya Kimataifa au mauzo ya Kimataifa ambayo yatakuwa yanatokea! Kinyume chake tunaweza tukalima, halafu tukasema mazao haya yanachukuliwa yanakwenda kuuzwa Kenya au yanakwenda kuuzwa wapi, kumbe yanapelekwa Ethiopia kwa sababu, watu wataangalia minada kule ikoje na huku wakulima wanaumiaje na kazi wanazozifanya; watakuja kuchukua mazao huku wapeleke huko!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba tu Serikali, kwa huu Muswada waliotuletea ni *excellent,* isipokuwa una tatizo moja tu! Hii Bodi, wasiwe hawa ndiyo wana dhamana ya kuuza mazao na badala yake iwe mamlaka ya mitaji na dhamana; basi ndiyo wawe na uwezo labda wa kutoa leseni. Hapa kidogo ndiyo naomba marakebisho hayo yawepo, hii inaweza ikatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niseme huu Muswada ni mzuri. Tatizo lake *impact* yake kuiona itakuwa ni vigumu sana kama hatutakuwa na *commodity exchange.* Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mwenyekiti: Mheshimiwa Bwanausi, jiandae Mheshimiwa Charles Kitwanga, Mheshimiwa Adam Malima na Mheshimiwa Zambi!

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi Ghalani. Haya nitakayoyasema ni maoni kutoka kwenye Jimbo langu la Lulindi, Wilaya ya Masasi, ambayo Wilaya hii ndiyo ya pili kwa uzalishaji wa korosho nchini. Kwa hiyo, mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani katika Wilaya ya Masasi ni mfumo ambao wananchi wengi wanautazama katika kuwaletea tija katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipoanzisha mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani ulikuwa na lengo zuri la kutaka kuwasaidia wakulima kuondokana na tatizo la soko la korosho, lakini kwenye utekelezaji wake kumejitokeza upungufu mwingi sana. Moja ya upungufu huo ambao wananchi wengi na wakulima wengi wa korosho wanalalamikia ni juu ya upataji wa malipo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikitangazwa bei dira 1,000 basi mkulima hupata 600/=! Hukaa tena miezi miwili mitatu anapata 400/= na baadaye anasubiri malipo ya majaliwa. Wakulima wanachotaka na wanachoona kwamba, ni lazima kifanyike na Serikali ni kupata malipo yao yote ya bei dira. Kama bei dira ni 1,000/= au 1,200/= basi ilipwe na baadaye asubiri malipo ya majaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limezungumzwa kwa muda mrefu sana, lakini bado Serikali kupitia Wizara zinazohusika bado haijaweka mkakati wa kuhakikisha jambo hili tunaliondoa kwa wakulima. Kwa hivyo, sasa hivi mfumo huu wananchi wanauona haufai kwa sababu ya utaratibu mbaya wa malipo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni juu ya makato yanayokatwa kwa mkulima. Makato ni mengi mno na ndiyo maana mkulima anaona kwamba, mfumo huu inawezekana unamgandamiza zaidi badala ya kumsaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu wananchi na wakulima wengi wanapenda mazao yao yauziwe kwenye maghala ya Chama chao cha Msingi. Kitendo cha kuondoa korosho zao na kupeleka kwenye maghala kilomita 200 au 300 kinawafanya kwanza kutokuwa na uwazi katika suala zima la biashara yenyewe! Kwa hiyo, huu utaratibu ambao Serikali inauandaa wa *Commodity Exchange*, hebu harakisheni basi! Kwa sababu umekuwa ni wa muda mrefu, zaidi ya miaka minne tunasikia *commodity exchange, commodity exchange* lakini hakuna kinachoendelea! Ziara za Watendaji wetu kwenda Ethiopia ni zaidi ya miaka miwili, tunajifunzaje miaka miwili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona kwa kweli, ni lazima utaratibu huu na Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* atueleze kwamba, huo mfumo wa *commodities exchange* unaanza lini? Ili wakulima huenda waone huo mfumo jinsi ambavyo utaweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Kamati katika mapendekezo yake imesema; pamoja na yote haya, lakini uongezaji wa thamani wa zao la korosho ndiyo suluhisho. Kule India ambako sisi tunapeleka korosho ghafi, hakuna viwanda vikubwa sana vya korosho! Kinachofanyika kule kuna viwanda vidogo vidogo vya wananchi ambao ni wa kipato cha kati ambao ndiyo wanabangua halafu wanapeleka kwenye viwanda vikubwa kwa ajili ya kumalizia hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kama Serikali haikuamua kufanya maamuzi magumu, jambo hili la kuongeza thamani hasa kwa zao la korosho, litakuwa gumu, kwa sababu, baadhi ya watu wanaonufaika na biashara hii hawawezi kukubali kuona mfumo huu

wa uthaminishaji wa zao la korosho ukifanyika hapa nchini! Kwa hiyo, naiomba Serikali suala hili lizingatiwe na lipewe umuhimu mkubwa, ili kuhakikisha wananchi wananufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema mkulima wa korosho sasa, hana maisha mazuri. Pamoja na kwamba, korosho ni zao ambalo linatuingizia fedha za kigeni na linawanufaisha watu wengi, lakini mkulima amebaki kuwa duni, mkulima amebaki kuwa ni mtu wa kunung'unika, badala ya kuneemeka kutokana na zao lake!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa dakika hizi chache ambazo umenipa nilitaka nichangie hayo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Napenda tu kwanza nitoe ufafanuzi kuhusu suala la makampuni kujiorodhesha katika *Dar-es-Salaam Stock Exchange*. Sheria Namba 14 ya Madini ya Mwaka 2010 inampa mamlaka Waziri anayehusika kutengeneza Kanuni zitakazowezesha kuyaweka katika *Dar-es-Salaam Stock Exchange* kwa kushirikiana na wadau, vile vile kwa kuhakikisha kwamba, wanafuata *Capital Market Authority Act. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiiangalia *Capital Market Authority* mahitaji yake! Tukaangalie makampuni yetu yaliyopo haya ya kati ambayo ni ya Watanzania ambayo yanaweza kuwa *listed* kwenye *Dar-es-Salaam Stock Exchange!* Tuangalie pande zote mbili kwa sababu, kuna mtu anayekwenda kununua *share* na kuna mtu anakwenda kutafuta mtaji kwenye *Dar-es-Salaam Stock Exchange!* Kwa hivyo, ni lazima Kanuni hizi ziwalinde watu wote hawa wawili na Kanuni hizi ziko tayari na Serikali inazo na inajadiliana na wadau husika, ili kuhakikisha kwamba, Kanuni hizi zinazotolewa, zitakazowekwa pale zinalinda sehemu zote mbili. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimpe Taarifa mzungumzaji kwamba, pamoja na kwamba, yeye ni sehemu ya Serikali, mimi sipo Serikalini! Kauli yake ya kwamba, hizo Kanuni zipo tayari, siyo sahihi, ni uwongo. Hizo Kanuni hazipo tayari kwa takribani miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama zipo tayari ziletwe hapa…

**WABUNGE FULANI:** Kufanya nini bwana! Kwani kanuni huwa zinaletwa hapa.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni zikiandikwa na Waziri zinakuwa *Gazetted!* Zinawekwa kwenye *GN!* Aseme ni *GN number* ngapi ambayo ina hizo Kanuni? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia Kanuni ziko tayari, lakini nimesema wazi kabisa, ni lazima ziendane na Sheria zingine za nchi kama Sheria ilivyosema. Kwa hiyo, Kanuni zilizo tayari ziko katika hatua ya kuchapishwa baada ya majadiliano na kuhakikisha kwamba, Sheria ya *Capital Market* vile vile inazingatiwa; tusije hapa kuzungumza vitu ambavyo ni vya kitaalam kisiasa! Wengine hapa tunazungumza mambo kitaalam tu, siasa hatuiweki mbele. Kwetu maslahi ya nchi na maslahi ya Watanzania wote ni muhimu zaidi kuliko maslahi ya watu binafsi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Malima, jiandae Mheshimiwa Zambi halafu Watoa Hoja mjiandae.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumzia ndani ya Bunge lako hili Tukufu. Jambo hili ambalo lina umuhimu wa kipekee kwa sekta ya kilimo kwa huko mbele kwa malengo tunayokwenda nayo. Nataka niseme tu kwamba, sisi siyo tuliobuni *Warehouse Receipt System,* mfumo huu umeanza miaka mingi na hata huko ulikoanza Marekani na maeneo mengine ulikuwa hautumiki kwenye kilimo! Kuna maeneo mengine ulikuwa unatumika hata kwenye *copper* na kadhalika na nini na lengo lake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilipotafsiriwa kwenye kilimo, *Warehouse Receipt System,* maana yake ni kumwezesha mkulima kuchukua mazao yake na kuyahifadhi kwa ajili ya kufanya kitu wanaita *hedging* au *Price Risk Managament*. Maana yake ni kwamba, unamwezesha mkulima kuwa na zao lile, kulihifadhi wakati kama bei inayumba, yeye anapata nafasi ya kupata bei iliyo nzuri zaidi pale itakapopanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakulima wengi hawana uwezo wa kuhifadhi mazao yao. Kwa hiyo, kwenye tafsiri ya *Warehouse Receipt System* kwenye mfumo wa kilimo au kwenye sekta ya kilimo, ni uwezo wa kumruhusu mkulima mdogo kuhifadhi mali yake akisubiri kupanda au kushuka kwa bei *(Price Risk Management)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachogomba kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani na mimi Adam Kighoma Malima ni mdau namba moja kwa sababu kwangu wakulima wangu ni wakulima kwa kiasi kikubwa wa korosho, sisi ndiyo tulifanyiwa majaribio na jambo hili. Kwa hiyo, akizungumza Mtutura, akizungumza Murtaza, nayajua ni kweli, lakini jamani tukubaliane hivi hasa hasa tumeumia sisi kwenye stakabadhi ghalani, sisi wakulima wa zao la korosho, tumeumia kwa sababu ya stakabadhi ghalani au tumeumia kwa sababu ya usimamizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usimamizi, hakuna usimamizi ambao unakosa Sheria na Sheria yenyewe ndiyo hii, sasa lazima tukubaliane, Mheshimiwa Mtutura anasema kuna kiongozi wa Ushirika alisema mjinga hajijui au kitu kama hicho, namkumbuka na namjua usiumize kichwa, kwangu mimi mwingine akaambiwa mjinga hajijui baada ya kuzikung'uta uzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi hao hao tulipokuja tukasema sasa mfumo huu wanaohujumu mfumo wa stakabadhi ghalani tuwachukulie hatua za kinidhamu kali, tuliruka kwa sababu wengine ndugu zetu. Sasa tunafanyaje? Anakuwaje mtu anayesimamia stakabadhi ghalani anasimamia mazao ya wakulima leo hata baiskeli inampa shida kununua baada ya miaka miwili ana mabasi matatu Newala na Tandahimba. Sasa tukubaliane tunataka nini, tunaacha nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbadala wa mfumo wa stakabadhi ghalani ni nini *chubuga, kangomba*, nani wote tunajua, sasa tukubaliane kwamba sisi ndiyo tunatengeneza Sheria, kama tunataka ukali wa kwenye sheria hii tuweke kwa sababu huko tunakozungumza Mheshimiwa Kafulila umezungumzia Eleni, Eleni nimefanya naye kazi wa *Commodity Stock Exchange,* aliyebuni *Commodity Stock Exchange* Ethiopia ni mama mmoja anaitwa Eleni anakuambia kule mtu anayechezea zao lile shiii, *gone*. Mtu anayechezea fedha ya wakulima, *gone* hakuna kubembelezana. Sasa *if that is what we want to make these things successful,* tufanye hivyo ili wakulima wetu, sisi ndiyo walinzi wa wakulima wetu, Serikali na ninyi, sisi wote Wabunge tukiona mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiko kwenye korosho, iko mpaka kwenye tumbaku, sasa tunafanyaje? Jamani tukubaliane na hakuna usimamizi, hiyo adhabu tunayotaka kuiweka kama hatuna Sheria tunaiweka kwenye nini? Lazima tuiweke kwenye nanihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme Mheshimiwa Arfi amezungumzia suala la mahindi na kadhalika. Mfumo wa stakabadhi ghalani msingi wake ni kutambua kwamba lazima pawe pana soko na *base* yake ni mambo matatu makubwa *warehousing,* la pili ni *marketing* na *marketing structure* yake ni ubora wa zao. Zao linapokosa ubora, *quality* ya zao ina maana hata huko nje hiyo pamba haiuziki, hayo mahindi hayauziki, hiyo korosho haitauzika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunahitaji *warehousing* yenyewe, lakini tunahitaji *quality* ya zao, halafu tunahitaji *financing,* hapo ndipo tutakapoingia sisi. Kwamba tunaingia kwenye *commodity exchange* ambayo inawekwa kwenye Sheria ya *commodity market,* lakini msingi wake ni kufanya kwamba mfumo wa fedha utambue sekta ya kilimo kama mhimili, mabenki na taasisi nyingine zisiogope mfumo wa kilimo. Sasa katika hilo Wabunge wataidai Serikali kwamba ni vipengele gani na hatua gani ambazo Serikali inachukua za makusudi kuhakikisha kwamba mkulima au ushirika unaokopesheka upate hiyo nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nakuomba kwa ridhaa yako, ukienda kuwasilisha zao lako unapewa kitu kinaitwa *warehouse receipt*. Ile *warehouse receipt* kwa mifumo ya wenzetu huko ni *negotiable instrument*. Ukishachukua ile *warehouse receipt* yako unaweza kwenda benki ukakopa. Ukichukua *warehouse receipt* unaweza kwenda ukanunua kitu, ukasema bwana, nakukabidhi *warehouse receipt* yangu ni hii, mazao yangu yako kadhaa, ukapata mali yako ukaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pale ndiyo kwenye uchache wa *system* yetu ambayo nawaomba Wabunge wote kwamba, tutambue kwamba, hayo matatizo na changamoto zilizokuwepo hazitopata ufumbuzi kama tusipopata Sheria kali na Sheria yenyewe ndiyo hiyo. Sasa kama Sheria haina ukali wa kutosha basi Mheshimiwa Kafulila tuitie moto zaidi, lakini ninachosema ni kwamba, mimi na wadau wa korosho na zao la korosho ndiyo zao lililoumia zaidi kuliko zao lolote katika mfumo wa stakabadhi ghalani lakini mbadala wake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba, nawasihi Wabunge wenzangu kwamba kwenye maeneo yale ambayo tunadhani stakabadhi ghalani kwa miaka minne, mitano iliyopita imekuwa na changamoto tuyazungumzie humu, tuyawekee utaratibu ambao kwanza kabisa unamlinda mkulima kwa mfumo huo huo, kwamba atapeleka zao lake na halafu lile zao tutambue kwamba Serikali siyo mnunuzi wa mazao, Serikali ni mlinzi wa wakulima. Sasa utaratibu wa kuamini kwamba Serikali ndiyo inanua korosho, inanunua mahindi, inanunua mpunga *is wrong,* sisi tunanunua akiba, lakini kwenye soko msingi wake ndiyo haya masoko yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama *the market are not working well,* lazima tuyafutie mfumo kama Serikali, kama Bunge wa kuhakikisha kwamba hii mifumo inakuwa kwanza ina maslahi ya kwanza kwa wakulima, halafu ndiyo iwe na maslahi kwa mabenki na watu wengine, lakini haiwezekani kwamba wakati mkulima anafanya biashara ya mazao mabenki kila siku yanapata faida na mkulima kila siku…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi angalau niweze kusema mambo machache kufuatia uwasilishwaji wa Muswada wa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Stakabadhi Ghalani, Sura ile ya 339.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Mheshimiwa Malima ambaye kwa sehemu kubwa amesema yale ambayo baadhi yake ningeweza kuyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema kwamba, utaratibu huu kwa wale ambao wanatoka kwenye maeneo hususan yale yanayolima kahawa ambako mimi nina uzoefu mkubwa sana, utaratibu huu wa stakabadhi ya mazao ghalani ulianza siku nyingi sana na wakulima kule walikuwa wanakusanya mazao yao kwenye maghala na hususan kahawa, wakisubiri bei, lakini pia wakati huo wakisubiri wayauze pamoja ili waweze kupata bei nzuri zaidi kwa wakati ambao siyo mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ule ulikuwa mzuri kwa sababu ulikuwa na nguvu na kulikuwa hakuna wanunuzi wengine ambao pia walikuwa wanaweza wakavuruga utaratibu ule wa stakabadhi ya mazao wa zao hilo la kahawa wakati huo. Huu ndiyo utaratibu ambao kwa sasa tunajaribu kuweka kwenye mazao mbalimbali na zao mojawapo pia ni korosho na tunakwenda kwenye mazao mengine ukiwemo labda mpunga, mahindi na mazao hayo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwasihi Waheshimiwa Wabunge, wengi wamezungumzia mfumo, sasa kwamba kuna kasoro kwenye mfumo, ndiyo sababu Mheshimiwa Waziri analeta hii Sheria ili iweze kuondoa kasoro ambazo zipo kwenye utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalani. Naomba niwasihi Waheshimiwa Wabunge, kwamba zile adhabu ambazo zimependekezwa katika mafungu mbalimbali ya *Amendment Bill* hii, nadhani zibaki vile vile kwa sababu wengi wamezungumzia kwamba kuna wizi na kuna mambo mbalimbali ya hovyo yanayowanywa na baadhi ya watu ambao kwenye vyama vya msingi na maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunaona huruma tena maana yake tunataka mwananchi huyu mkulima aendelee kuumia. Kwa hiyo, ili watu hawa ambao wanahusika labda na *management* ya maghala yenyewe lakini kwenye Vyama vya Msingi kwenye Vyama vya Ushirika waweze kushika adabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu zinazopendekezwa naomba zibaki vile vile, Serikali inafanya hivi kwa maslahi ya mkulima na siyo kwa maslahi ya wale wachache ambao wanajinufaisha kwa manufaa yao na Mheshimiwa Mtutura amezungumza vizuri. Sasa watu wa namna hiyo kama wapo wezi, tusiwaonee huruma na haya ndiyo tunayoyazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria yenyewe ya 2005 iliyotungwa ilikuwa na changamoto adhabu ndogo, mambo mengine hayakukaa vizuri ndiyo haya tunataka tuya-*address*. Sasa tunapotaka tuya-*address* na tuweke sheria na faini ambazo zinaweza zikawabana hawa watendaji wanaohusika, basi nadhani ni vizuri mkaruhusu zibaki kama ambavyo imependekezwa kwenye Sheria yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme haya yafuatayo:-

Tunajenga maghala ili kuwezesha mfumo huu uweze kufanya kazi vizuri. Chini ya Wizara ya Kilimo tuna maghala karibu 275 na ambayo tayari tumeshaanza kuyajenga na pesa zimeanza kupatikana na katika kipindi cha miaka mitatu tunategemea maghala yote 275 yawe yameshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunayapeleka jirani zaidi na wananchi ili tuhakikishe kwamba mazao yao yanaweza yakatunzwa pale, yakakusanywa pale na kama ambavyo imeshaelezwa, basi wakaweza kupata soko zuri zaidi na la uhakika, kuliko likiachwa sasa hivi

lilivyo na huko nyuma tunajua kulikuwa na soko holela hapo katikati ndiyo tunakuja na utaratibu huu ili kuweza ku-*address* baadhi ya changamoto hizi ambazo kimsingi zinajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini limezungumzwa suala la kwamba wakulima wanalazimishwa kupeleka mazao kwenye Vyama vya Ushirika. Kimsingi Ushirika ni hiari, hakuna mkulima ambaye analazimishwa kuingia kwenye Ushirika lakini chini ya utaratibu huu, mkulima mmoja mmoja kimsingi hawezi, ndiyo pale anapolazimika kupitia kwenye Ushirika ili aweze kuuza mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme imeelezwa kwamba hivi faida zipi zipo za kuingia kwenye utaratibu huu. Zipo faida nyingi, nisemee tu kwenye korosho yenyewe. Mwaka 2007/2008, bei ya korosho ilikuwa kwenye shilingi mia mbili, mia tatu haikuzidi mia nne, lakini mpaka leo baada ya kwenda kwenye utaratibu huu tunavyou-*perfect* kila mara, sasa hivi bei ya korosho inafika mpaka shilingi elfu mbili chini ya utaratibu huu huu wa stakabadhi ya mazao ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaouza kupitia utaratibu mwingine kwa mfano *kangomba* na nini bado wanauza chini ya bei hiyo na wanafanya hivyo kwa sababu hiyo hela wanaipata mara moja, sidhani kama kuna faida kubwa kwamba leo unapata faida kwa mara moja halafu ukasubiri miezi labda mwezi mmoja, miwili ukaona tabu sana…

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Zambi kwamba, tuliposema kwamba, kuna tatizo la kuwalazimisha watu wapiti Vyama vya Msingi ili waweze kuweka mazao yao kwenye ghala, tunamaanisha kwamba wapo watu ambao wanao uwezo wa kuweka mazao yao kwenye ghala hiyo bila kupitia Chama cha Msingi ili kuepuka ghalama ambazo mkulima anaziingia kwa kupitia utaratibu wa Chama cha Msingi.

Kwa hiyo, tunachokisisitiza hapa Mheshimiwa Zambi ni kwamba, watu wenye uwezo wa kuweka mazao yao kwenye ghala bila kupitia Chama cha Msingi wanakataliwa, ndiyo hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba Serikali iseme tu kwamba, sasa waruhusiwe na ichukue hatua kwa wanaokataliwa, hawa wanaowakataza hayo mamlaka wanatoa wapi wakati Sheria haipo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naomba niseme kwamba, hakuna mwananchi anayelazimishwa kupeleka mazao yake kwenye Ushirika na mwananchi huyu kama ana mazao yake mengi anaweza akayatunza na akaruhusiwa kutafuta soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme sasa hivi pia tumeruhusu kutoa vibali kwa mwananchi ambaye anaweza akakusanya mazao yake, lakini tuhakikishe kwamba anaweza kulipa kodi za Serikali na baadaye akaweza kuyauza. Utaratibu huu unatumika pia kwenye mazao kama korosho na mazao ya kahawa ambapo wengine hawalazimiki hata kupita kwa mfano, kwenye mnada kule Moshi kwa maana ya kahawa. Kwa hiy, mtu akipata kibali anaruhusiwa, sijaona kama kuna mtu amesema lazima apitie hapa, hatujafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba, kimsingi utaratibu huu una faida zaidi kuliko hasara. Kama zipo kasoro zinazojitokeza, ndiyo sababu tunaleta Muswada huu. Tu–*address* changamoto hizo ili mkulima huyu ambaye tunamkusudia aweze kupata faida. Naomba niseme kwamba sisi wote humu ndani ni *product* au ni watoto wa mkulima, ungekuwa

mtoto wa mfanyakazi, mfanyakazi huyu pia vyovyote vile lazima anakula mazao ya kilimo, atahusika na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kimsingi wote tuna uchungu na wakulima na Serikali hii ina uchungu na wakulima na ndiyo sababu tunaleta mambo ambayo yanamkusudia, mambo mazuri kwa huyu mkulima. Sidhani kama kuna Serikali yoyote ambayo inamkusudia mwananchi wake mambo mabaya. Kwa hiyo, tunafanya hivi kwa manufaa ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu wanasema kwamba mkulima huyu anafaidikaje na bei, yaani kwenye bei hizi zinavyopangwa anafaidika namna gani? Utaratibu wa sasa kwa mfano, kwenye korosho tuna utaratibu wa minada. Kwenye minada kule wakulima wenyewe kupitia Vyama vyao vya Ushirika, wanahudhuria hiyo minada. Kwa hiyo, bei inapotangazwa mnadani, wana hiari wenyewe kwamba, tunaridhika na bei au haturidhiki na bei hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo ambalo liko wazi na nitashangaa sana kwamba kuna mkulima ambaye anaambiwa korosho yako utauza shilingi mia mbili au shilingi mia tano bila yeye mwenyewe kuhusika. Hii siyo kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme pamoja na muda mfupi ambao siyo mrefu sana wa kuwa Wizarani lakini moja ya maeneo ambayo nimejitahidi kujifunza kwa haraka ni sekta ya korosho ambayo nimejitahidi pia kufika katika maeneo mengi ambayo wanalima korosho. Zipo changamoto tunakubali, lakini ndiyo hizi ambazo tunaendelea kuzi-*address*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa ni vibali vya mazao mbalimbali. Vibali vya kuingiza baadhi ya bidhaa nchini vinatolewa kwa utaratibu maalum. Ziko Kamati ambazo zinaangalia, kwa mfano, kama ni sukari inaangalia kwamba sukari haitoshi, basi wanaruhusu na sukari hii tunaiingiza mara moja tu katika kipindi cha mwaka kwa sababu tuna uwezo wa kuzalisha sukari wenyewe, lakini tunakuwa na *gap* karibu la miezi mitatu nchini ambayo sukari tunayozalisha nchini haikidhi, kwa hiyo, pale tunaweza tukatoa kibali cha kuingiza sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi tumeshatangaza zabuni kwa ajili ya kuingiza karibu sukari kama tani laki moja ambayo ni kati ya mwezi wa Nne, wa Tano, wa Sita na baadaye mwezi wa Sita viwanda vinapoanza kuzalisha sukari nchini, tunakuwa tumefunga hatuendelei tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali hivi vinatolewa kwa uwazi na hakuna mizengwe ambayo inatumika, sasa kama kuna mambo mengine yanayoendelea ya magendo, ndiyo changamoto ambazo Serikali inaendelea kuzifanyia kazi kwa sehemu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hili la mazao ya wakulima kukopwa. Hili tumeshalisema mara nyingi sana. Mheshimiwa Waziri ameshalisema hapa na tumeshasema nia njema ya Serikali ilikuwa ni kuchukua mazao ya wananchi kuliko kuyaacha mengi mikononi mwao na wananchi wengi tulikuwa kimsingi tumekubaliana nao kwamba tutachukua mazao yao halafu baadae tuwalipe na tulikuwa tunadaiwa zaidi ya bilioni 112, sasa hivi tumeshalipa zaidi ya bilioni 90 na zimebaki karibu bilioni 45 ambazo na zenyewe zipo katika hatua mbalimbali za malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza kuna malipo ambayo yanaendelea kufanyika na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametuahidi kwamba inawezekana wiki ijayo akatoa hela nyingine na ni matumaini yetu kwamba, ndani ya kipindi kifupi kinachokuja, basi tuwe tumemaliza madeni ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la wananchi kuibiwa fedha za tumbaku. Tumepata mchango kwa maandishi, wakulima wanapoibiana kwenye Vyama hivi tunataka watupe Serikali taarifa, pale ambapo hatuna taarifa ni vigumu sana kuchukua hatua. Ilitokea kwenye tumbaku tumefanya kazi kubwa *CAG* alikwenda kule tumepata taarifa na wale wote waliohusika sasa hivi *IGP* anashughulika nao kwa ajili ya kuhakikisha kwamba anawapeleka Mahakamani ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia ya Serikali kwa kweli kuhakikisha kwamba, vitendo vya wizi kwenye mazao ya akulima kupitia kwenye Ushirika vinaweza vikakomeshwa ili ushirika ambao tunao uonekane ni wa manufaa kwa mkulima, kuliko adhabu zaidi kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba niseme ningependa kuchangia katika maeneo haya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge nina tangazo dogo, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi anaomba kuwatangazia Wajumbe wake wote kuwa leo saa saba mchana kutakuwa kuna kikao Msekwa C.

Mheshimiwa Waziri, mtueleze vile vile malalamiko haya ya sukari, yanaleta mgogoro mkubwa sana. Wadau wa sukari wanalalamika, mnaagizia sukari wakati sukari bado ipo nchini, tupeni taarifa sahihi.

Pili, kuna malalamiko kuwa watu wanaagizia sukari ya viwandani lakini wanachanganya na sukari ya kuuzwa na inaingia mitaani bila kulipa kodi. Hebu tupeni usahihi wa taarifa hizi, siyo leo, jiandae huna sababu ya kutoa jibu, lakini mjiandae mtupe taarifa sahihi. Mheshimiwa Naibu Waziri!

Pia hili la Wabunge wanalalamika wote, kuna neno la kiingereza linatamkwa Kiswahili linaitwa *(MBWA - Management By Walking Around)*. Tunaomba jamani mwende huko kwenye stakabadhi ghalani na wengine wamesema kuna maua ya korosho yameshaanza kutoka, wananchi wanapata tabu sana huko.

Mheshimiwa Naibu Waziri, njoo hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala zima la mfumo huu kuwa hautasaidia wakulima kwa sababu ya utendaji wake. Nafurahi kuwa hata Kambi ya Upinzani wamekubali kuwa huu mfumo ukisimamiwa vizuri, utaleta ufanisi katika masuala mazima ya mauzo ya mazao ya wakulima wetu.

Sasa kama ni suala utendaji, ndiyo maana ya Muswada huu. Huu Muswada umeletwa kwa sababu ya kurekebisha upungufu uliokuwa katika Muswada uliopita ambao vilevile uliibuliwa humu ndani pamoja, kwa wakulima na wananchi kwa ujumla na huu Muswada umejaribu sana kujibu kwa kiasi kikubwa sana masuala haya.

Mfumo huu unazungumziwa kuwa unaongeza mzigo kwa wakulima. Nataka kusema kuwa kwa vyovyote vile mkulima hawezi kukwepa kabisa gharama zote, lakini zile ambazo ni za ziada ambazo siyo za lazima tutaziangalia na kwenye Muswada imeonyeshwa kabisa kuwa hakuna mtu atakayebebeshwa mzigo zaidi ya ule. Kuna mapendekezo yametolewa hapa kuhusiana na kwamba kuna gharama fulani kwa mfano za *shrinkage* zile zisirudi kwa mkulima. Hilo tutaliangalia, tutaweka *percentage* ngapi kila zao ambayo ni *allowable* kwa ajili ya

*shrinkage,* hiyo mkulima hatarudishiwa kama gharama kwake, itaendelea kubebwa na yule anayehusika na kutunza lile ghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la kusema kuwa eti hakuna maslahi yoyote ambayo yamepatikana kwa wakulima hasa wa korosho kwa sababu naona hilo la korosho ndiyo limepigiwa kelele sana, mimi nataka kupiga kuwa siyo kweli. Wakulima wamefaidika huu mfumo, kama kuna upungufu huo ndiyo tuufanyie kazi na ndiyo maana ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei imepana kutoka Sh. 450/= hadi Sh. 1,300/= kwa kupitia mfumo huu huu. Korosho zilisemekana kuwa ni za daraja la pili, la tatu; sasa hivi zimekuwa za daraja la kwanza kwa sababu zinasimamiwa vizuri kwa kuwekwa katika maghala kwa ufanisi zaidi. Wananchi wa Tunduru bei yao vilevile imelinganishwa na inaonekana pia ni nzuri kwa wakulima hawa. Kwa hiyo, kama kuna mtu anaona kuwa hili siyo sawa, basi kwa kweli bora angetoa mapendekezo mazuri zaidi kuliko kulaumu na kukandia moja kwa moja.

Kulikuwa kuna suala zima la kulazimisha Vyama vya Ushirika, nashukuru kuwa Mheshimiwa Zambi amelijibu. Nafikiri hilo limeeleweka.

Mheshimiwa Arfi amesema kuwa huu Muswada hauna msaada yoyote, lakini vilevile bado anauliza wakulima wangapi wamefaidika? Haraka haraka nimwambie tu, ni zaidi ya wakulima 572 wa Vyama vya Ushirika vya Msingi wamepata mikopo kwa miaka saba kwenye zao la korosho peke yake. Wakulima wa vikundi na Vyama vya Msingi zaidi ya 320 kwenye zao la kahawa, vikundi na wakulima 120 kwenye zao la mpunga, Vyama zaidi 12 kwenye zao la mahindi. Hayo ni manufaa!

Kulikuwa kunazungumziwa mambo ya ufisadi. Mheshimiwa Kafulila, sasa umekuwa ni wimbo kwako, kila ukisimama, ufisadi, *commodity exchange*! Ufisadi, *commodity exchange!* Kila tukikusikia unazungumzia suala hili hili tangu tuanze.

Nataka kukufahamisha Mheshimiwa Kafulila na Waheshimiwa Wabunge wengine wote kwamba *commodity exchange* itaanzishwa, sasa hivi iko kwenye Baraza la Mawaziri. Nataka vilevile nikufahamishe kuwa *commodity exchange* haiwezi kuanza kabla ya kuwa na mfumo rasmi ambao unatambulika ambao umekaa kisayansi utakaozingatia ubora wa mazao na mfumo wa kielektroniki wa mauzo.

Kwa hiyo, suala la maghala lazima yawepo, suala zima la kuweka *receipt system* lazima iwepo. Wewe mwenyewe ulisema Ethiopia walianza na *commodity exchange* wakajikuta kuwa wataenda kuuza kitu gani? Hakiko! Kiko wapi? Huwezi kuweka mazao kwenye majumba ya watu halafu ukayauze *internationally*. Hujui ubora wake, hujui *grade* yake, hujui kiasi chake, haiwezekani! Ni lazima tuanze kwenye msingi wa *commodity warehouse receipt system then we move to commodity exchange* na hiyo pia nayo iko tayari kwa taarifa yako, itaanza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kafulila nafikiri itabidi utafute wimbo mwingine tu sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *commodity exchange* tumeanza mchakato wake 2011, 2006 ilikuwa ni *warehouse receipt*. Nenda kwenye kumbukumbu zako wewe ni *lawyer* unajua kukariri miaka. Nataka kujibu sasa hoja zote zilizotolewa kwa ujumla kwenye Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchelewa kuanzisha soko la mazao ya bidhaa nimeshalijibu, soko hilo linaanzishwa sasa, limefikia katika ngazi la Baraza la Mawaziri. Kanuni zilikuwepo kwa sababu tayari tulikuwa tuna Muswada. Huu Muswada siyo mpya, tunaurekebisha. Kanuni zilikuwepo, sasa hivi tutaziboresha kufuatana na huu Muswada mpya jinsi utakavyopitishwa.

Kwa hiyo, kanuni zipo na mwaka huu zitakuwa tayari kwa sababu ni suala tu la kuziboresha siyo mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya korosho vilikufa siyo kwa sababu ya stakabadhi ghalani, ni kwa sababu ya teknolojia iliyokuwa ikitumika imepitwa na wakati na sasa hivi kuna viwanda vipya vinne vya korosho ambavyo vitakuwa na mfumo wa kisasa wa kiteknolojia ya kisasa utakaowezesha mauzo ya korosho kuwa bora zaidi. Kwa hali hiyo, hivyo viwanda hata vikirudishwa itabidi vikarabatiwe upya, havitarudi katika mfumo ule uliokuwepo mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo litazungumzwa katika mada nyingine, hapa tuko kwenye kuzungumzia Muswada, samahani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la soko la mazao na bidhaa, tunaambiwa kuwa upangaji wa bei au dira hufanywa bila kuzingatia bei ya Soko la Dunia, lakini hii siyo kweli. Waheshimiwa wakati mwingine tunapotoa michango, tutoe michango ambayo kwanza ina tija, lakini vilevile na sisi wenyewe itatulinda.

Upangaji wa bei na dira hufanywa kwa kuzingatia bei ya Soko la Dunia na gharama za uzalishaji. Baada ya Kamati ya bei kupendekeza bei, hujadiliwa katika mikutano ya wadau na kukubaliwa.

Kwa hiyo, wakulima huwa wanahusika na wanafahamu kwa kupitia Vyama vya Ushirika hata wao wenyewe mmoja mmoja. Takwimu tulizonazo sasa ni kwamba kutokana na Mfumo wa Stakabadhi Ghalani bei zinapatikana kubwa, nzuri zaidi kuliko ilivyokuwa mwanzo wakati soko lilikuwa linajiendesha kiholela.

Kuhusiana na faida, hii ni kujibu suala la Kamati. Faida za mfumo tulizielezea kwa makini kwenye Kamati, lakini naamini Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, atalijibia. Kulikuwa na suala la *Collateral Manager*, tuliulizwa kuwa hii haijatolewa katika Muswada? Lakini nataka kuwafahamisha kuwa imetolewa katika sehemu ya (h) ya Muswada *Collateral Manager, definition* yake na ufafanuzi juu ya kazi zake na wajibu wake na masharti mengine yanayohusu *Collateral Manager* yapo katika Muswada huu ambao tunaupendekeza sasa hivi.

Kuhusiana na Kamati katika ngazi ya Mkoa na Wilaya, marekebisho yalivyoainishwa na Waheshimiwa katika Kamati ya Bunge, yamefanyika na hivi sasa itasimamiwa na Katibu Tawala badala ya ma-*DC* Wakuu wa Mikoa. Kwa hiyo, hili nalo tumeshalifanyia kazi, kwa hiyo, kama kulikuwa na suala lolote la wasiwasi kuwa litakuwa la kisiasa, sasa hivi litakuwa kiutendaji zaidi.

Mheshimiwa Mkapa amependekeza kuwa ingekuwa bora wakulima wakalipwa japo nusu. Mfumo huu kwa uhalisia wake unatakiwa utoe *advance* kwa mkulima anapoleta mazao yake kwenye ghala. Anaweza hata kulipwa asilimia 100 iwapo watakuwa tayari kupeleka mazao ghalani bila kukopa Benki. Lakini wanapokopa Benki inabidi sasa kiasi kingine kibakie kama vile *guarantee* fulani au *insurance*, kuwa kama mkulima asipoweza kulipa, basi yale mazao yake nusu yake yanaweza yakatumiwa kulipia lile deni lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa jukwaa la kuuza mazao litaongeza sana ufanisi katika soko la mazao yetu. Naamini kama kuna upungufu wowote sisi ndio tunapaswa kuusimamia na kuhakikisha kuwa unafanyika.

Kulikuwa kuna suala la adhabu. Adhabu zile Waheshimiwa zinawalenga wale wale ambao mnawalalamikia kuwa wanawalangua wakulima. Mtambue kuwa hili ni kundi la watu ambao matajiri, wana-*influence* kubwa, tukiwatoza faini ndogo ndogo hivi haviwazuii kufanya

wanayoyafanya. Ndiyo maana tumeweka adhabu kali kwa ajili yao na wakati mwingine tumechanganya mpaka na kufungwa ili waache kunyonya wakulima wetu. Sasa nashangaa mnarudi tena hapa mnatuambia tupunguze zile adhabu. Wakati mnajua kabisa kama hawa ni watu ambao wamekuwa wakivuruga soko kwa kuwanyanyasa wakulima wetu na bei zao.

Kwa hiyo, naomba hili suala la adhabu libakie kama lilivyo katika Muswada kwa sababu hata hivyo tumeshapunguza. Tulikuwa tunazungumzia asilimia 150, lakini Kamati imependekeza tufanye 50 na ndiyo hiyo amayo tumekubaliana nayo na hiyo milioni 20 siyo kitu kwa watu wenye kununua mazao wakubwa ambao tunawafahamu.

Mheshimiwa Huvisa amezungumzia kuwa changamoto kubwa ni utendaji na kwa kweli hilo lilionekana na ndiyo maana Muswada huu umeletwa sasa kuboresha na ku-*tight*en zile *screw* pale ambako utendaji ulikuwa umelegalega.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka kuwaomba Waheshimiwa mpitishe Muswada huu kwa sababu sasa ndiyo unazingatia haya masuala mnayosema ya utendaji.

Mheshimiwa Mtutura nakuomba tu ndugu yangu, kaka yangu, tumetoka mbali, ubadilishe mawazo, uunge mkono hoja Muswada huu na yale yote ambayo yana upungufu tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu mimi ni hayo machache, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Viwanda na Biashara!

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa michango ambayo tumeipata kutoka kwenye Kamati yetu ya Fedha na Uchumi, lakini vilevile michango iliyotoka kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, sijui kama nina haja ya kuwatambua; yupo Mheshimiwa Arfi, Mheshimiwa Mtutura, Mheshimiwa Barwany, Mheshimiwa Kafulila, Mheshimiwa Mkapa, Mheshimiwa Mangungu, Mheshimiwa Luoga, Mheshimiwa Suzan Kiwanga, Mheshimiwa Zuberi, Mheshimiwa Bwanausi, Mheshimiwa Kitwanga, Mheshimiwa Malima, Mheshimiwa Zambi, pamoja na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara kwa kutanguliwa na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Kitandula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuwaasa Waheshimiwa Wabunge wenzangu waelewe kwamba Muswada huu haukuwekwa katika hali hii na Wizara ya Viwanda na Biashara peke yake, Muswada huu umepitia tanuri zito sana.

Kamati ya Fedha na Uchumi imeuangalia kwa kina, Kamati ya Kilimo imeuangalia kwa kina, na kama isitoshe kuna wadau mbalimbali wameangalia Muswada huu, *ANSAF* wameuangalia, Chuo cha Sokoine wameuangalia, *CMSA* wameuangalia, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Taasisi za Haki za Binadamu, Bodi ya Korosho na baadhi ya Wawakilishi wa Wakulima, wote tumeupitia huu Muswada. Mimi nina-*appreciate concern* zilizotolewa hapa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kuelezea udhaifu uliojitokeza kutokana na mfumo mzima wa stakabadhi za ghala.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwahakikishieni kwamba kazi kubwa iliyofanyika katika kupitia Muswada huu, imeangalia kwa karibu sana upungufu uliokuwepo tokea sheria hii itungwe mwaka 2005 na kuanza kutumika baada ya kanuni zake kutokea mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kwamba tunapozungumzia Muswada huu, tuelewe kwamba sasa ndiyo mwarobaini wa kuondoa hizi kero tunazozingumzia sasa hivi. Kwanini nasema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ukiusoma ule Muswada wa Stakabadhi za Ghala baada ya uzoefu huu, tumeona wazi kabisa hakuna utaratibu rasmi hata ule wenyewe wa kuuza kwenye ghala kwa mwenye mali, hata wale Wakala, hata wale wahifadhi wenyewe. Kulikuwa hakuna utaratibu, kulikuwa hakuna *incentives* zozote, tuliweka Kamati mbalimbali, Kamati zile zilikuwa hazina nguvu yoyote, hazikuwa zikitambulika kisheria, usimamizi ulikuwa mgumu hata katika ngazi ambazo zingewajumuisha wakulima wenyewe.

Mwanzo tuliweka awepo Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya tukasema lisije likawa ni suala la kisiasa, sasa tumemweka *RAS* na Mkurugenzi wa Maendeleo ili liwe la kitaalam. Vile vile hata hiyo Bodi inayozungumzwa, kazi yake kubwa ilikuwa ni kutoa leseni tu; unatoa leseni unaondoka, lakini sheria hii imetoa pia na udhibiti wa utoaji ule wa leseni kwamba Bodi hizi zinapata nguvu ya udhibiti na zina mamlaka ya kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, udhibiti huu siyo tu kwa wakulima, lakini kwa wale wadau wakuu, hata wale *Financial Institutions,* maana walikuwa wanafanya tu mambo yao bila kuwa na udhibiti wowote. Kwa hiyo, kulikuwa hakuna utaratibu ambao ulikuwa unasimamia uendeshaji wa stakabadhi za ghala kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tuangalie hata kwenye ile sheria iliyopita, zile adhabu zilizokuwa zinatolewa. Adhabu zenyewe zilikuwa wala siyo *substantive*. Kwa hiyo, kama kuna watu ambao siyo waadilifu wanaweza kufanya taratibu tu ambazo zikawa ni athari kwa wakulima wakasema kwanza adhabu yenyewe ni Sh. 10,000/=. Sasa katika hali hii kwa kweli Muswada huu umehakikisha kabisa hata viwango vya adhabu vinakuwa ni vile ambavyo vitafanya watu kutokukiuka utaratibu uliowekwa katika mfumo huu mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za haki sasa zitakuwa za uhakika, tunaunganisha sasa na mitandao ya kibenki, na kwa sababu hiyo tunakwenda mpaka vijijini inawezekana kabisa mitandao hii ikagusa mpaka maeneo ya vijiji. Lakini vilevile tunafanya utaratibu kwa sababu tunataka kwenda ki-*electronic* kuunganisha na mtandao wa Kimataifa kwa maana ya kukuza soko letu. Vilevile itatupa taarifa sahihi. Taarifa sahihi siyo Serikalini tu, hata Bungeni tutapata taarifa sahihi sasa, lakini vilevile kuhakikisha ubora wa mahindi yale yanayouzwa katika utaratibu huu wa stakabadhi za ghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kabisa kwamba eneo moja ambalo lazima tulisimamie ni eneo la usimamizi na utendaji. Hilo ni lazima tukubaliane kwamba tulipe msisitizo mkubwa sana. Nasi sasa tumeanza katika hali hiyo kwa sababu tayari, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla, tayari sasa hivi tuna mkakati wa kuleta Muswada wa *commodity exchange,* umekwishafika kwenye Baraza la Mawaziri na Muswada ule utaombewa kujadiliwa katika Bunge la Bajeti lijalo. *Analysis* kubwa imefanyika na Wabunge wenyewe kuuelezea mfumo huu na baadhi ya Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sioni haja ya kwenda tena kwenye *details* ambazo tayari zimeshatolewa na Kamati, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia hapa, vilevile na baadhi ya Mawaziri waliochangia hapa. Ninachosema, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuchukue marekebisho ya sheria hii kama alivyosema Mheshimiwa Barwany, iwe sasa ni mwarobaini wa kuliweka suala hili sawa ambalo mwanzo ingawa lilikuwa linafanyika, lakini kulikuwa na upungufu mkubwa wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishaweka kisheria sawasawa, kwa hali yoyote ile usimamizi wake utakuwa ni mzuri. Vilevile hii ni njia mojawapo ambayo Serikali ikisaidiana na Bunge na wadau mbalimbali tunatambua tatizo, lakini hapo hapo na kujua ufumbuzi wake ni nini.

Mimi niwahakikishieni sheria sasa iliyotungwa kama alivyosema Mheshimiwa Mangungu na wengine ni nzuri kazi kubwa ya Serikali itakuwa ni usimamizi ili tupunguze hizi kero ambazo wote ni wadau. Kwa sababu sheria hii kwa kiwango kikubwa inawagusa wakulilma ambao tunataka tuwafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Kilimo unaweza ukazungumzia mambo mengi; ukazungumzia masoko, bei; naomba *focus* yetu kwa sasa tuone kwamba stakabadhi za ghala *as a price seeking mechanism,* tunaiboresha vipi ili mkulima aweze kupata bei nzuri lakini hapo hapo tukitengeneza *platform* ya kuelekea kwenye utaratibu mzima wa *commodity exchange*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa maelezo machache, vilevile kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tupitishe sheria hii, tuimarishe usimamizi, tukawasaidie wakulima ambao wamepata adha kubwa kwa kiasi fulani katika utaratibu wa kutafuta bei ya mazao yao wanayozalisha huko Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi Ghalani wa Mwaka 2014**
***(The Warehouse Receipts (Amendment) Bill, 2014)***

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 7
Ibara ya 8

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12

Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwenye ibara hiyo nilipenda kiongezeke kifungu ambacho kitakuwa na namba (g) kwa maana kwamba pamoja na mambo mengine, mwendeshaji wa biashara hii ni lazima aweke bima dhidi ya majanga, dhidi ya upotevu na uharibufu mwingine ambao unaweza ukatokea kwa mazao ambayo yatakuwa yamehifadhiwa na mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanyika hivi itasaidia sana kuondoa utaratibu uliopo sasa kwamba hasara nyingine yoyote inayotokana na uhifadhi wa mazao anabebeshwa mkulima, jambo ambalo siyo sahihi na halistahili kufanyika hivyo. Kwa hiyo, nilipenda kwamba tuongeze hicho kifungu ili kuondoa tatizo hilo ambalo limekuwepo kwa siku zote.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali. Ni wazo zuri tu kuwa na *insurance*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Mheshimiwa Mangungu na Serikali)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26

Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33
Ibara ya 34

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta mapendekezo kwamba kwenye kifungu hicho kiongezeke kifungu ambacho kitatoa uhuru kwa mkulima kuweza kufanya mauzo vile ambavyo atakuwa yeye mwenyewe ameamua. Kusiwe na utaratibu wa kum-*bind* mkulima kwamba ni lazima apeleke katika utaratibu wa ghala hata kama hajafikia kiwango kile cha kuweza kupeleka kwenye ghala.

Kwa hiyo, nilikuwa nimependekeza kwamba tuongezee kipengele hapa ili iwe ni jambo la kuchagua, aidha apeleke katika utaratibu huo au apeleke kwenye utaratibu mwingine ambao yeye mwenyewe atakuwa anaona unafaa, pamoja na usimamizi wa Serikali ili kusiwe kuna taratibu wa kuwadhulumu wakulima kwa namna nyingine yoyote. Ahsante.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo sasa ni kwamba kwa kweli mkulima yupo huru kuuza mazao yake popote pale anapohitaji mradi tu afaute sheria na taratibu na kanuni zilizopo. Tunachofanya Serikali ni tunahakikisha kwamba hawadhulumiwi.

Vilevile kwa utaratibu huu kama tulivyozungumzia, tumesema ni utaratibu wa kutafuta bei nzuri, *price seeking mechanism* kwa mkulima, lakini kwamba auze mahali popote sidhani kama hiyo imekuwa ni kikwazo kikubwa sana. Sasa kutia kwenye sheria au kutokutia, sijui kama itakuwa ni *semantic* tu, lakini hata likiingia kwenye sheria hapa, halitaathiri kitu chochote, linaweza likaingia tu, lakini ndiyo hali ilivyo. Nilitaka kuongea hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, umekubali?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Mheshimiwa Mangungu)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi Ghalani wa Mwaka 2014**
***(The Warehouse Receipts (Amendment) Bill, 2014)***

(*Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi Ghalani wa Mwaka 2014 *(The Warehouse Receipts (Amendment) Bill, 2014* ibara kwa ibara pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria wa Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii kazi ya Bunge imekwisha. Sasa imebaki shughuli hii iende kwa Mheshimiwa Rais ili aweze kuridhia na hii sasa iwe sheria kamili. Napongeza sana Wizara kwa kazi nzuri mliyofanya, nakupongeza Mwanasheria Mkuu kwa ushauri ambao mnautoa mzuri Bungeni, lakini napongeza Wabunge kwa ushirikiano mzuri ambao mmeutoa na hasa kufanikisha zoezi hili.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 5. 48 Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 23 Machi, 2015 Saa Tatu Asubuhi)*